# CHANGAMOTO KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA SOMO LA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA: UCHUNGUZI KIFANI WILAYA YA TEMEKE

**NEEMA SAMUEL NDOMBA**

**TASNIFU INAYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA KUTIMIZA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA ISIMU (M.A. ISIMU)**

**IDARA YA ISIMU NA TAALUMA ZA FASIHI**

**CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2023**

## UTHIBITISHO

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania inayoitwa; **Changamoto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili katika Shule za Sekondari Tanzania: Uchunguzi Kifani Wilaya ya Temeke,** katika utimilifu wa sehemu ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili (MA-Kiswahili).

………………………….………

Dkt Zelda Elisifa

(Msimamizi)

…………………….….……..

Tarehe

## HAKI MILIKI

Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kuigwa, kukaririwa, kunakiliwa, kuhifadhiwa kwa njia yoyote au kuwasilishwa kwa mbinu yoyote ile; ya kielektroniki, kunakili, kurudufu katika hali yoyote bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

# TAMKO

Mimi, **Neema Samuel Ndomba**, natamka na ninathibitishwa kwamba tasnifu hii inayoitwa: "Changamoto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili katika Shule za Sekondari Tanzania: Uchunguzi Kifani Wilaya ya Temeke; ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawai kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kingine kwa ajili ya kutunuku shahada kama hii au nyingine yoyote.

……..……………………..………

Sahihi

……………………..………

Tarehe

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa familia yangu; mume wangu Sauli Epimack John na watoto wetu Trinity (Bula), Trixie (Hanji) na Tivan (Lae) kwa kuniunga mkono na ustahimilivu wao nilipoanza safari ya somo yangu haya.

## SHUKURANI

Awali ya yote natoa shukrani zangu za dhati na za pekee kwa Mwenyezi Mungu muumba mbingu na vyote kwa kunipa uhai, uzima na uwezo wa kuweza kuandika na kukamilisha kazi hii. Kwa hakika bila msaada wake lolote haliwezi kufanyika.

Pili shukurani zangu za pekee zimwendee msimamizi wangu mpendwa, Dkt. Zelda Elisifa, kwa kutumia muda wake kwa hali na mali katika kunitia moyo nilipoonekana kukata tamaa. Licha ya mapungufu niliyokuwa nayo aliweza kunivumilia, akapitia kazi yangu, akaisahihisha na kuelekeza vilivyo ili kuhakikisha kuwa inakuwa inavyotakiwa kuwa. Nakiri kuwa nimejifunza mengi kutoka kwake. Mafanikio ya tasnifu hii yametokana na juhudi yake kubwa ya kusoma, kukosoa, kurekebisha, kuelekeza na kushauri yale yote yanayofaa kuzingatiwa. Sina cha kumlipa ila nakuomba kwa Mungu azidi kukupa maisha marefu na mema ili uendelee kutoa mchango kwa watafiti wengine.

Ninashukuru Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa Idara ya Isimu na Taaluma za Fasihi wakiwemo walimu wangu Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Dunlop Ochieng, Dkt. Hadija Jilala na Dkt. Bakar Kombo kwa mihadhara na maelekezo mbalimbali iliyoniongezea maarifa zaidi katika shahada hii. Vilevile shukurani za pekee ziwafikie mume wangu Sauli Epimack John na watoto wetu Trinity(Bula), Trixie(Hanji) na Tivan(Lae) kwa ushirikiano mkubwa wa maombi na uvumilivu waliokuwa nao nilipokuwa nasoma, kuna wakati walinihitaji lakini kutokana na majukumu ya usomaji na kazi hii haikuwezekana.

Mwisho niwashukuru watafitiwa kwa kukubali na kutenga muda wao kushiriki katika utafiti huu, bila wao data muhimu za utafiti huu zisingepatikana.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari wilaya Temeke. Lengo la utafiti lilikuwa kutathmini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke na malengo mahususi yalikuwa ni kutathmini changamoto za upatikanaji wa nyenzo za kufundishia kwa walimu wa somo la Kiswahili, kuchunguza changamoto za upatikanaji na matumizi ya nyenzo za kujifunzia, kutathmini ubora wa maandalizi ya walimu kuhusu ufundishaji na kubainisha maoni ya watafitiwa kuhusu utatuzi wa changamoto walizoibua. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Utabia inayosisitiza upataji na mabadiliko ya uwezo wa tabia inayotokana na michakato ya ujifunzaji na mazoea yanayoimarishwa. Sampuli ya utafiti ilikuwa watafitiwa 120, (wanafunzi 100, walimu 15 na wakuu wa shule 5) kutoka shule tano katika kata ya Mibulani. Mbinu ya unasibu ilitumika kuwateua. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia njia ya usaili na mahojiano. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na kitakwimu. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa suala la nyenzo za kufundishia bado ni tatizo. Pia upatikanaji na matumizi ya nyenzo za kujifunzia ni tatizo linalowakabili wanafunzi. Utafiti umebaini mafunzo kwa walimu ni suala ambalo halipewi kipaumbele katika kuimarisha ufundishaji. Ilibaini kuwa nyenzo za kufundishia na kujifunzia bado ni tatizo ambalo lina kwamisha ufundishaji na ujifunzaji. Utafiti unatoa mapendekezo kwa serikali na wakuu wa shule kuhakikisha upatikanaji na uenezaji wa nyenzo za kujifunzia na kufundishia. Walimu wa Kiswahili waongezewe mafunzo ya kuimarisha ujuzi wao kwa kupitia warsha au semina.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ......................................................................................... **ii**

**HAKI MILIKI** ......................................................................................... **iii**

**TAMKO** ......................................................................................... **iv**

**TABARUKU** ......................................................................................... **v**

**SHUKURANI** ......................................................................................... **vi**

**IKISIRI** ......................................................................................... **vii**

**YALIYOMO** ......................................................................................... **viii**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ......................................................................................... **xii**

**ORODHA YA UFUPISHO** ......................................................................................... **xiii**

**SURA YA KWANZA** ......................................................................................... **1**

**UTANGULIZI** ......................................................................................... **1**

1.1 Usuli wa Mada ......................................................................................... 1

1.3 Malengo ya Utafiti ......................................................................................... 9

1.3.1 Lengo kuu ......................................................................................... 9

1.3.2 Malengo Mahususi ......................................................................................... 9

1.4 Maswali ya Utafiti ......................................................................................... 10

1.5 Umuhimu wa Utafiti ......................................................................................... 10

1.6 Mipaka ya Utafiti ......................................................................................... 11

1.7 Vikwazo vya Utafiti ......................................................................................... 11

1.8 Hitimisho ......................................................................................... 12

**SURA YA PILI** ......................................................................................... **13**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI** ......................................................................................... **13**

2.1 Utangulizi ......................................................................................... 13

2.2 Dhana za Lugha, Ufundishaji, Ujifunzaji, Lugha ya Kufundishia na Nyenzo ............ 13
2.2.1 Lugha ............ 13
2.2.2 Ufundishaji ............ 14
2.2.3 Ujifunzaji ............ 14
2.2.4 Lugha ya Kufundishia ............ 15
2.2.5 Nyenzo za Kufundishia ............ 16
2.3 Mapitio ya kazi Tangulizi ............ 16
2.4 Kiunzi cha Nadharia ............ 20
2.5 Pengo la Utafiti ............ 25
2.6 Hitimisho ............ 25
**SURA YA TATU ............ 27**
**MBINU NA NJIA ZA UTAFITI ............ 27**
3.1 Utangulizi ............ 27
3.2 Usanifu na Mkabala wa Utafiti ............ 27
3.3 Eneo la Utafiti ............ 28
3.4 Sampuli na Usampulishaji ............ 29
3.4.1 Kundi Lengwa ............ 29
3.4.2 Sampuli ............ 29
3.4.3 Usampulishaji ............ 30
3.5 Mbinu za ukusanyaji wa Data ............ 32
3.5.1 Hojaji ............ 33
3.5.2 Mbinu ya Usaili ............ 34
3.6 Hitimisho ............ 35

**SURA YA NNE** ........................................................................................36

**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA** ................................................36

4.1 Utangulizi ........................................................................................36

4.2 Changamoto za Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundishia ..............................36

4.2.1 Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundishia ......................................................36

4.2.2 Sababu Zinazoathiri Uteuzi wa Nyenzo za Kufundishia Somo la Kiswahili ........................................................................................39

4.2.3 Idadi ya Matumizi ya Nyenzo za Kufundishia .............................................40

4.3 Upatikanaji na Kiwango cha Matumizi ya Nyenzo Za Kujifunzia ...............41

4.3.1 Upatikanaji wa Nyenzo za Kujifunzia ........................................................41

4.3.2 Kiwango cha Matumizi ya Nyenzo za Kujifunzia ......................................42

4.4. Maandalizi katika Ufundishaji ....................................................................44

4.4.1 Maandalizi Kabla ya Kuingia Darasani .......................................................45

4.4.2 Mahudhurio ya Semina au Warsha Juu ya Ufundishaji ...............................45

4.4.3 Idadi ya Mahudhurio Semina au Warsha .....................................................47

4.4.4 Umuhimu wa Mafunzo...................................................................................47

4.4.5 Changamoto katika Maandalizi ya Ufundishaji ...........................................47

4.5 Maoni ya Walimu, Wanafunzi na Wakuu wa Shule Kuhusu Somo la Kiswahili ........................................................................................49

4.5.1 Maoni ya Wanafunzi Juu ya Somo la Kiswahili ..........................................50

4.5.3 Maoni ya Wakuu wa Shule ..........................................................................56

4.6 Hitimisho .........................................................................................59

**SURA YA TANO .......................................................................................... 61**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................ 61**

5.1 Utangulizi ............................................................................................. 61

5.2 Muhtasari wa Utafiti ............................................................................. 61

5.2.1 Muhtasari wa Jumla ............................................................................ 61

5.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ....................................................... 62

5.3 Hitimisho .............................................................................................. 64

5.4 Mapendekezo ya Utafiti ....................................................................... 65

5.4.1 Mapendekezo ya Kiutekelezaji ........................................................... 65

5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Nyingine ........................................................ 66

**MAREJEO ..................................................................................................... 68**

**VIAMBATANISHO ....................................................................................... 74**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 4.1 Upatikanaji wa nyenzo za kufundishia ..................................................37

Jedwali 4.2 Sababu zinazoathiri uteuzi wa matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa somo la Kiswahili.........................................................39

Jedwali 4.3 Idadi ya matumizi ya nyenzo za kufundishia ........................................40

Jedwali 4.4 Upatikaji wa nyenzo za kujifunzia.........................................................41

Jedwali 4.5 Matumizi ya nyenzo katika ujifunzaji wa somo la Kiswahili................43

Jedwali 4.6 Mahudhurio ya semina au warsha .........................................................46

Jedwali 4.7 Idadi ya mahudhurio ya warsha na semina............................................47

Jedwali 4.8 Changamoto katika maandalizi ya ufundishaji......................................48

Jedwali 4.9 Changamoto ambazo hukumbana nazo wakati wa ujifunzaji................51

Jedwali 4.10 Kauli zifuatazo kuhusiana na somo la Kiswahili.................................52

Jedwali 4.12 Mapendekezo ya suluhisho za changamoto.........................................55

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| NECTA | National Examinations Council of Tanzania |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| WEMA | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1Usuli wa Mada

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Ufundishaji ni mchakato unaohusisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi au kati ya mwanafunzi wenyewe. Riley (2005) anafafanua kuwa kujifunza ni tendo la kuwasilishwa kwa hali ya jambo halisia na lisilo halisia. Hivyo, tunapojifunza ni lazima wanafunzi walegwa kulijua somo na Ujifunzaji wa lugha una hatua, kanuni na taratibu zake. Kwa hiyo, mwanafunzi anatakiwa kufundishwa kanuni na misingi ya lugha husika ili aweze kuielewa lugha.

Hata hivyo, baadhi ya wataalamu wa elimu ya ujifunzaji lugha akiwemo Skinner (1957) anaamini kuwa mtu hujifunza lugha kama anavyojifunza tabia yoyote ile kama vile kukimbia, kuimba na kutembea. Skinner, anaona ujifunzaji wa lugha ni mwigo, na kuwa ni uimarikaji wa tabia. Hivyo mtoto mdogo hazaliwi na lugha bali huichota kutoka kwa wazazi wake na watu wanaomzunguka. Skinner anasisitiza kuwa tendo la kujifunza ni tabia na hivyo kujaribu na kukosea ni sehemu ya mchakato wa kujifunza. Naye Wilga Rivers (1968) anasisitiza kuwa, mtoto hujifunza kupitia kujaribu na kukosea (“trial and error’) na huendelea kufanya hivyo mpaka anapofikia matamshi ya jamii nzima.

Mtazamo wa Skinner unatofautiana na mitazamo ya baadhi ya wataalamu wa lugha kuhusu ujifunzaji wa lugha. Noam Chomsky (1957), wazo lake kuu ni kua watoto au binadamu huzaliwa wakiwa na mfumo wa lugha katika ubongo, hivyo binadamu

huzaliwa akiwa na uwezo wa lugha, yaani kwenye ubongo wake ana mfumo ambao huzaliwa nao kwa ajili ya kujifunza lugha. Chomsky anafafanua kuwa ujifunzaji wa lugha ni lazima uhusishwe na maelekezo ya kanuni za lugha ambao ndio msingi wa kujifunza.

Kwa ujumla mawazo ya Skinner yamejikita zaidi katika uamiliaji wa lugha yaani mwigo kuliko ujifunzaji wa lugha, hivyo inapaswa ieleweke kuwa kuna tofauti kidogo kati ya ujifunzaji wa lugha na uamiliaji wa lugha; kwani mbinu za ujifunzaji wa lugha hutofautiana na zile za uamiliaji wa lugha. UNESCO (1953)inaeleza kuwa kuamilia lugha sio sawa na kujifunza lugha.Watoto huamilia lugha kwa kuiga wanachosikia kutoka kwa jamii inayowazunguka,huwa na mwitikio wa vichochoe na hufuatisha mifumo yote sawa na wafanyayo watu wengine wanaowazunguka na wanapofanya makosa hutegemea marekebisho na wasipokoselewa huchukulia wako sahihi na hubaki na kile walichokiiga kama ndio sahihi. Lakini kwa mtazamo wa Chomsky, ingawa mtoto amezaliwa na uwezo lakini anahitaji kanuni za ufundishaji wa lugha kwani kuna umri fulani hawezi kupata lugha sawasawa na wazawa wa lugha hiyo. Kwahiyo ufundishaji lazima utawaliwe na kanuni mbalimbali na mwanafunzi lazima azifuate.

Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha una historia ndefu duniani. Kwa mujibu wa Richards & Rodgers (1986), suala la ufundishaji na ujifunzaji lugha lilianza kutiliwa mkazo katika nchi za kimagharibi mapema katika karne ya 14 wakati Kilatini kilipokuwa lugha pekee ya matumizi katika shughuli za biashara, elimu, dini na utawala. Hata hivyo katika karne ya 16 lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kitaliano zilianza kutambulika kwa sababu ya mabadiliko ya kisiasa. Mwishoni mwa karne ya

17, wanaisimu mbalimbali walianza kutathmini mitazamo mbalimbali ya ufundishaji wa lugha kuanzia ile ya asili ya kutafsiri sarufi hadi ile ya moja kwa moja ambapo mkazo ulikuwa kuzungumza kuliko kuandika. Richards & Rodgers (1986) wanaendelea kueleza kuwa mitazamo hii ilifuatiwa na uundaji wa jedwali la kifonetiki za kimataifa mwaka 1886 ili kuwezesha unukuzi sahihi wa sauti za lugha yoyote duniani.

Mabadiliko ya teknolojia yalipoanza yaliathiri sekta ya elimu duniani, na kufanya walimu kuongeza shauku ya kujua nyenzo za ufundishaji ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. Mwalimu anapaswa kuamua kwa kuchagua kwa makini njia na nyenzo bora za kufundishia ili wanafunzi wake waweze kujifunza kwa ufanisi. Misingi ya kuchagua nyenzo ni kuzingatia, umri wa wanafunzi na malengo ya somo katika kufundishia na kujifunzia. Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari unatakiwa kuwa jambo la kuzingatiwa kwa sababu ya hadhi mpya ya Kiswahili duniani. Mabadiliko ya nyenzo za ufundishaji na ujifunzaji yanatakiwa ili kuweza kukidhi haja iliyopo kwa wanafunzi kwa sababu Kiswahili ni lugha miongoni mwa lugha zinazosomwa na kufundishwa ulimwenguni kwani Kiswahili kinafundishwa katika vyuo vikuu vya kimataifa katika bara la Asia, Ulaya na Amerika ya kaskazini. Mfano katika Bara la Amerika ya Kaskazini katika nchi ya Marekani, baadhi ya vyuo hufundisha lugha ya Kiswahili kwa wazawa na wageni. Vyuo hivyo ni Minnesota, Harvad, Texas na Michigani.

Kwa mujibu wa Muhtasari wa Somo la Kiswahili Kenya (1985), nchini Kenya, lugha ya Kiswahili ni somo la lazima katika elimu ya msingi na ya upili. Kembo-Sure (1996) anasema kuwa, kulikuwa na mabadiliko makuu katika sekta ya elimu ya

Kenya, Kiswahili kilipopewa hadhi kwa kuteuliwa kuwa somo la lazima darasani na hata katika mitihani. Hii inatokana na Kiswahili kutambuliwa kuwa na uzito sawa kama Kiingereza katika kuendesha masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katiba mpya ya Kenya iliyozinduliwa mwaka 2010 iliikweza nafasi ya lugha ya Kiswahili zaidi kwa kuitambua kama lugha rasmi.

Vilevile Kiswahili kinafundishwa kama somo katika vyuo vikuu kuanzia shahada ya kwanza hadi ngazi ya uzamivu, baadhi ya vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Kenyatta na Nairobi. Shitemi & Mwanakombo (2001) wanasema, Kiswahili kinapiku lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kienyeji katika kutimiza malengo ya kitaifa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Sababu ni kuwa kimatumizi, Kiswahili hukiuka mipaka ya kikabila, na matabaka kiuchumi na kielimu. Kiswahili huwawezesha Wakenya wengi kushiriki katika masuala ya maendeleo katika jamii. Nchini Tanzania lugha ya Kiswahili ilianza kutiliwa mkazo kabla ya uhuru kwani watawala katika shughuli zao za kampeni za siasa na uchumi walitumia lugha ya Kiswahili na hatimaye lugha hiyo ilianza kutumiwa katika shughuli za kielimu nchini.

Msokile(1992) anasema wakati wa utawala wa Mjerumani (1884-1914) waliweza kuruhusu Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia darasa la 1-4. Na hata wakati wa utawala wa Mwingereza waliendelea kutumia Kiswahili kama somo kwa darasa la 1-4. Pia katika ngazi ya elimu ngazi ya kati (middle school) Kiswahili kilitumika kama somo. Anaendelea kufafanua kuwa, hata baada ya uhuru 1965 Kiswahili kilifanywa kuwa lugha ya kufundishia katika shule za msingi kwani wizara ya elimu ilihimiza utungaji wa vitabu vya Kiswahili vyenye kuzingatia siasa na utamaduni wa Watanzania.Sera ya Elimu na mafunzo Tanzania (2014) inafafanua kuwa Lugha ya

Kiswahili ni lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu ya Tanzania kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya msingi na pia inafundishwa kama somo katika kiwango cha sekondari hadi chuo kikuu.

Ingawa Kiswahili ni somo katika shule za sekondari, bado kinakumbana na changamoto za wingilugha. Kwa sasa suala la wingilugha limekuwa jambo lisiloepukika katika mawasiliano baina ya watu kutoka mataifa mbalimbali kwa sababu ya maendeleo ya kiuchumi, kielimu, kisiasa na kibiashara. Kiswahili ni lugha rasmi ya taifa, pia ni lugha ya kufundishia kwa shule za awali na za msingi (isipokuwa chache ambazo hutumia lugha ya Kiingereza). Kutokana na umuhimu huu, Sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 inatamka wazi kuwa serikali itahakikisha kuwa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na nyingine za kigeni zinafundishwa kwa ufasaha na ufanisi katika ngazi zote za elimu na mafunzo nchini ili kuleta ufahamu wa umahiri kutokana na umuhimu wa lugha hizo katika masuala ya kimataifa (WEMU 2014).

Suala hili limezua mjadala kati ya wanaisimu na wataalamu wengi wa elimu kwa sababu hali hii imesababisha wanafunzi wa sekondari kutotilia mkazo kujifunza somo la Kiswahili kwa sababu wamelipa umuhimu mdogo kulinganisha na lugha nyingine za upili kama Kiingereza na Kifaransa. Mbaabu&Nzunga, (2008) wanabainisha kwamba kasumba mbaya na mtazamo hasi wa Watanzania katika lugha ya Kiswahili imekuwa ni changamoto katika ufundishaji wa somo la Kiswahili kwani wanafunzi wa sekondari hutilia mkazo lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa, kwa sababu hiyo ufaulu wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari umekuwa na changamoto. Naye Swilla (2009) anathibitisha kwamba Watanzania

wanakosa moyo wa kuthamini na kujali tamaduni zao ambapo Kiswahili ni lugha inayotangaza utamaduni wao lakini wao wanathamini sana utamaduni wa kimagharibi. Kwa hakika hii ni changamoto kubwa ambayo inakabili somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Rubagumya (1990) anaeleza kwamba, makampuni ya kigeni hayahitaji wafanyakazi ambao wanashindwa kutumia lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa kama lugha za mawasiliano. Kwa kufanya hivyo kumekuwa na mwitikio duni wa wanafunzi kutilia mkazo ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

Hoja hiyo imeungwa mkono na Mukhawana (1995) katika utafiti wake kuhusiana na ujifunzaji lugha kwani alibaini kwamba, matumizi ya lugha nyingine zinazotumika kufundishia mashuleni kwa mfano Kingereza na Kifaransa, zimetengeneza ushindani na mtiririko duni wa wanafunzi kupenda somo la Kiswahili. Mwinshekhe(2003), katika utafiti wake alibaini kwamba matumizi ya lugha za kigeni katika kufundishia yamechangia kwa kiasi kikubwa wanafunzi kutopenda somo la Kiswahili hivyo kupelekea wao kufanya vibaya.

Masamba (2004) anadai kwamba pamoja na hadhi na umaarufu wa Kiswahili, bado lugha ya Kiswahili inakumbana na matatizo makubwa ya zana na matumizi ya lugha hii na kusababisha ufaulu hafifu wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari. Balisidya (1987) katika utafiti wake wa zana za kufundishia somo la Kiswahili alieleza kwamba zana za kufundishia ni lazima ziwe na sifa ya kusadifu mada, ionekane na iwe na uwezo wa kuhifadhika. Mpaka sasa tafiti mbalimbali zimebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika eneo la ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari. Kutokana na ukweli huo, mtafiti aliona haja ya

kuzidi kutathmini changamoto za ujifunzaji na kugusia pia ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa sekondari kwani kulikuwa na ombwe linalohitajika kuzibwa kwa sababu watafiti wengi wameibua changamoto katika ufundishaji, mfano changamoto ya wingilugha katika ufundishaji lakini hakuna aliyedokeza changamotoza katika nyenzo za ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili katika kukuza umilisi wa lugha kwa wanafunzi. Vilevile utafiti huu ulienda mbali zaidi kwakuangalia changamoto zinazowakabili wakuu wa shule katika kuhakikisha ufaulu kwa wanafunzi na mwamko kwa walimu wa somo la Kiswahili. Kwani kwa kuzibaini zinavyoathiri suala zima la ujifunzaji na ufundishaji zitaleta suluhisho na kuimarisha mwamko zaidi wa walimu katika ufundishaji na wanafunzi katika usomaji.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu kikatiba nchini Tanzania. Matharani somo la Kiswahili ni la lazima katika shule za sekondari kuanzia kidato cha 1-4. Hali hii imefanya Kiswahili kuwa mojawapo ya somo ambalo Mwanafunzi anatakiwa kupata kuanzia alama ya C kupanda juu (A na B) katika mtihani wake kwa kuhitimu elimu ya sekondari ndipo ajiunge na masomo ya ngazi za juu. Na Wanafunzi wasioweza kupata alama ya C katika somo la Kiswahili huathiri nafasi zao za kujiunga na viwango vya juu katika kuendelea kujifunza somo hilo.

Hivyo ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili ni muhimu sana katika kumwezesha mwanafunzi kupata umilisi wa kisarufi na umilisi wa kiufundi ili kuweza kufikia malengo yake ya kielimu. Mwalimu wa somo la Kiswahili anayo nafasi ya kutumia nyenzo zenye lengo la kumwezesha mwanafunzi kufikia malengo.

Ingawa kuna matumizi ya nyenzo na mahudhurio ya semina au warsha kwa Walimu, bado ufaulu wa Wanafunzi ni hafifu na husababisha athari katika ufaulu kwa wanafunzi. Hali hii imemsukuma mtafiti kuchunguza zaidi juu ya upatikanaji wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia na mahudhurio ya semina au warsha kama changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari.

Besha (1994) aliyechunguza changamoto za ufundishaji na ujifunzajikatika shule za sekondari Simanjiro na kulibaini kwamba athari za lugha ya kwanza ni changamoto kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili. Pia Mbunda (1996) alitathmini changamoto za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na alibaini kwamba wanafunzi wa sekondari hawathamini somo la Kiswahili na badala yake huchukulia kama somo la kuwasaidia kufanya mawasiliano na thamani kubwa hupewa lugha ya Kiingereza.

Pia Saleh (2019) katika tasnifu yake, alichunguza changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni katika darasa mseto la wingilugha na alibaini kwamba walimu hawana taaluma na ujuzi wa kuweza kuyajua mahitaji ya wanafunzi wao kabla na wakati somo linaendelea, hivyo akapendekeza ni vyema kwa walimu kujifunza tabia mbalimbal za wanafunzi ili kupunguza changamoto ambazo zitawatokea. Naye Akaka (2013) aliangazia changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini kenya, utafiti wake ulibaini idadi kubwa ya walimu wanaoajiriwa kufundisha katika shule hizi changa, hawana tajriba ya kufundisha katika kiwango hili.

Matokeo ya tafiti hizi yamedhihirisha kuwa changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji zinaathari kubwa katika matokeo ya mwanafunzi katika ujifunzaji wake.

Tafiti nyingi zimeangazia walimu na wanafunzi, hivyo basi utafiti ulijumuisha kundi jipya katika utafiti. Hata hivyo, hakuna utafiti wowote ambao umetathmini maoni ya wakuu wa shule kama sehemu ya kundi lengwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari. Vilevile hakuna utafiti ulifanyika katika wilaya ya Temeke katika kutathimini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili ambapo wanafunzi wengi wanaonyesha kuwa na ufaulu hafifu wa somo la Kiswahili kulinganisha na wilaya nyingine za mkoa wa Dar es Salaam.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na aina mbili za malengo, yaani lengo kuu na malengo mahususi.

### 1.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kutathimini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari Wilaya ya Temeke.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi yalikuwa:

i. Kutathamini changamoto za upatikanaji wa nyenzo za kufundishia kwa walimu wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke.

ii. Kuchunguza changamoto za upatikanaji namatumizi ya nyenzo za kujifunzia kwa wanafunzi wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke.

iii. Kutathmini ubora wa maandalizi ya walimu kuhusu ufundishaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke.

iv. Kubainisha maoni ya walimu, wanafunzi na wakuu wa shule kuhusu utatuzi wa changamoto za somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke.

**1.4 Maswali ya Utafiti**

Maswali ya utafiti huu yalilenga kuchunguza yafuatayo:

i. Ni changamoto gani za upatikanaji na matumizi ya nyenzo za kufundishia kwa walimu wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke?

ii. Kuna changamoto gani kwa wanafunzi katika kupata na kutumia nyenzo za ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke?

iii. Walimu hujiandaa kwa ubora upi kuhusu ufundishaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke?

iv. Ni nini maoni ya walimu, wanafunzi na wakuu wa shule kuhusu utatuzi wa changamoto za somo la Kiswahili katika shule za sekondari za Temeke?

**1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu utakuwa na umuhimu kwa wadau mbalimbali wa elimu. Wanufaika wa kwanza ni walimu kwani utafiti huu utatoa mwanga kwao katika maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili na utaongeza maarifa mapya kwa wasomi na waalimu wanaofundisha somo la Kiswahili. Matokeo na mapendekezo yaliyotolewa yatawawezesha waalimu na wanafunzi kupenda ufunzaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa njia inayostahili. Mtafiti anataraji kuwa, matokeo ya utafiti huu yatachangia katika elimu ya Kiswahili kwa kuwawezesha waalimu na wanafunzi kujua namna ya kulikabili somo la Kiswahili. Hali kadhalika, matokeo ya

utafiti huu yatakuwa msingi bora kwa kutoa maelekezo kuhusu jinsi ya kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika eneo la utafiti. Utafiti huu utashawishi watafiti wengine na kutumika kama rejea katika kuendeleza mada hii.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu uligusa changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari wilaya ya Temeke. Mtafiti aliangazia suala la ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Kiswahili kwa Walimu na Wanafunzi wa Somo la Kiswahili. Hivyo watafitiwa walikuwa walimu wa somo la Kiswahili, wanafunzi wa kidato cha tatu na sio madarasa mengine kwa sababu ndio darasa ambalo hutumia nyenzo kwa kiwango kikubwa na hawabanwi na ratiba ya mtihani na majaribio ya mara kwa mara kulinganisha na kidato cha pili na kidato cha nne. Matokeo ya utafiti yamewakilisha changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari Tanzania.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na na vikwazo kadhaa, vikwanzo hivyo ni kama:

i. Baadhi ya watafitiwa kukataa kufanyiwa usaili kwa kuhofia usiri wa taarifa, hivyo mtafiti ilimlazimu kuwaakikishia kutunza siri kwa kuheshimu maadili ya utafiti kwa kuwa utafiti huu una madhumuni ya taaluma na sio vinginevyo, na kwa kuzingatia hilo zaidi mtafitiwa hakulazimika kuandika jina lake wakati wa usaili.

ii. Ratiba ya shule ilikuwa kikwazo, ratiba ya ukusanyaji data iliingiliana na ratiba za majaribio na kumlazimu mtafiti kufanya ziara siku nyingine katika eneo la utafiti ili kuweza kuwapata watafiwa.

## 1.8 Hitimisho

Sura hii imebeba mwongozo wa sura zinazofuata kwa kutoa utangulizi na kubainisha mambo yaliyofanyiwa utafiti ikiwemo tatizo la utafiti, malengo, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti, mipaka, vikwazo pamoja na hitimisho

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imetathimini maandiko ya kinadharia na ya kazi tangulizi.Marejeleo ya vitabu na machapisho yanayohusiana na mada hii ya utafiti huu yamehusika.Sura hii inaonesha mtazamo wa wataalamu mbalimbali kuhusiana na mada hii ya utafiti.Sehemu ya kwanza ni utangulizi,ikifuatiwa na dhana muhimu katika utafiti, kisha mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia. Mwishoni, pengo la utafiti vimenyeshwa.

## 2.2 Dhana za Lugha, Ufundishaji, Ujifunzaji, Lugha ya Kufundishia na Nyenzo

Dhana muhimu katika utafiti huu zimefasiliwa ili kumfanya msomaji aweze kuelewa kwa haraka. Dhana hizo ni Lugha, Ufundishaji, Ujifunzaji, Lugha ya kufundishia na Nyenzo za kujifunzia.

### 2.2.1 Lugha

Wataalamu mbalimbali wameifafanua lugha kwa namna zinazotofautiana kwa kiasi kidogo sana, na wafuatao ni miongoni mwa wataalamu hao. Mtaalamu Barber (1972) anasema kuwa "lugha ni utaratibu wa kupeana ishara unaotumia alama za sauti. Ni utaratibu unaotumiwa na kundi maalumu la watu kwa nia au madhumuni ya kuwasiliana kwa haja ya kushirikiana katika jamii".Weber (1985) anafasili kuwa "lugha ni mfumo wa mawasiliano ya binadamu ambao hutumia mpangilio maalumu wa sauti kuunda vipashio vikubwa zaidi. Kwa mfano, mofimu, maneno na sentensi". Pia anadai kuwa lugha ni mfumo wowote wa mawasiliano ya watu kwa mfano lugha ya Kifaransa na lugha ya Kihindi. Hivyo basi, kulinganana maelezo ya wataalamu

hao, lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zilizo katika mpangilio maalum zenye kuleta maana inayokubaliwa na wanajamii fulani na wenye utamaduni mmoja ili zitumike katika mawasiliano miongoni mwao.

### 2.2.2 Ufundishaji

TUKI (2004) inafasii ufundishaji kama namna ya kufundisha au kuelekeza mtu jambo ili alifahamu. Chacha (2016) anaongeza kwamba mbinu za kufundishia ni muhimu katika ufundishaji wenye kuleta matokeo mema, na kwamba ni muhimu kutilia mkazo mbinu za ufundishaji wa somo la Kiswahili kwani italeta manufaa kwa walengwa. Walimu wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali katika shughuli zao za kila siku. Kulingana na Sitanda (1980) na Chacha (2016), ujifunzaji hutegemea na jinsi mwalimu alivyotayarisha njia za kufundishia.

Hivyo, ufundishaji ni jumla ya vitendo vya maandalizi ya somo linalokusudiwa, matumizi ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vitendo vya mwanafunzi katika harakati za kujifunza na jukumu la mwalimu kinadharia na vitendo katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwahiyo Ufundishaji hudhamiria kuwasaidia watu kujifunza. Na sababu kuu ya mwalimu kufunza ni ili mwanafunzi wake apate kuelewa kwa kupata mwelekeo chanya na maarifa yanayofaa kulingana na lengo kuu la somo.

### 2.2.3 Ujifunzaji

Riley (2005) anafafanua kuwa kujifunza ni tendo la kuwasilishwa kwa hali ya jambo halisia na lisilo halisia. Massamba (2004), anasema kuwa ujifunzaji lugha ni utaratibu wa kufanya jitihada rasmi za kuijua na kuitumia lugha fulani. Mtu yeyote

ana uwezo wa kujifunza lugha na kuifahamu ikiwa tu atakuwa na akili timamu pamoja na ala sauti zote zinazohusiana na ujifunzaji lugha. Hivyo, tunapojifunza ni lazima kujua somo na wanafunzi walegwa. Ujifunzaji wa lugha una hatua, kanuni na taratibu zake. Kwa hiyo, mwanafunzi anatakiwa kufundishwa kanuni na misingi ya lugha husika ili aweze kuielewa lugha.

### 2.2.4 Lugha ya Kufundishia

Lugha ya kufundishia ni lugha inayotumiwa na mwalimu kufundishia wanafunzi Zhou na Sun (2004). Aidha, lugha ya kufundishia ni lugha iliyoteuliwa kutolea elimu kwa taifa zima au sehemu ya taifa na kwa kiwango maalum cha elimu au kwa viwango vyote vya elimu. Msanjila na wenzake (2009) wanadai kwamba lugha ya kufundishia ni lugha inayotumiwa kutolea maarifa katika mfumo wa elimu. Naye Qorro (2006) anatoa hoja kwamba lugha ya kufundishia ni chombo cha kupitishia elimu kutoka kwa walimu kwenda kwa wanafunzi na miongoni mwa wanafunzi wenyewe. Hali kadhalika, Qorro (2005), anafafanua kwamba pale wanafunzi wanaposhindwa kuongea lugha ya kufundishia hakika hawataweza kujifunza.

Vilevile Msanjila na wenzake (2011), wanasema kuwa lugha ya kufundishia inapoteuliwa visivyo, huwa kunajitokeza vikwazo vingi ambavyo huathiri ufanisi katika kutoa, kubuni na kuendeleza maarifa. Vikwazo hivyo ni wajifunzaji kuwa na mtazamo wa kutoipenda lugha hiyo, kuondoa juhudi za kuijua na kuitumia, hivyo kukwamisha michakato ya ujenzi na utoaji wa maarifa muhimu kwa maendeleo ya jamii. Kwahiyo, ili wanafunzi wapate maarifa na uwezo wa kujitambua na kung’amua kile kilichofundishwa na mwalimu wake lazima awe na umilisi wa lugha ya kufundishia. Kwa jumla, lugha ya kufundishia inapaswa kuwa ni ile inayotumiwa

na watu wengi katika mawasiliano yao ya kila siku kama ilivyo kwa Kiswahili.

### 2.2.5 Nyenzo za Kufundishia

Ayot (1986) anasema kuwa, nyenzo za kufundishia ni zana za kufundishia na kujifunzia zinazowasaidia walimu katika ufundishaji na uimarishaji wa ujifunzaji. Mawazo haya yanaungwa mkono na Wright (1976) anaposema kuwa, vyombo vya kufunza na kujifunzia ni muhimu sana kwa sababu wanafunzi hupata habari zaidi kutokana na vyombo hivi kuliko kutoka kwa walimu. Mwalimu anapopanga atakayofundisha, mikakati ya ufundishaji lazima aambatanishe nyenzo za kufundishia ambazo huhusisha somo atakalofundisha. Eshiwani (1983) anasisitiza kwamba matokeo mazuri katika shule za sekondari yanaweza kuhusishwa na kuwapo kwa nyenzo na matumizi yake katika somo. Kulingana na matokeo hayo, mwalimu wa lugha ya Kiswahili anahitaji kuwa na nyenzo za kutosha za kufundishia ambazo zitatumika ipasavyo na wanafunzi katika kuongeza ufaulu zaidi. Nyenzo zikitumiwa vizuri, humsaidia mwanafunzi kutekeleza jambo kikamilifu na kuelewa dhana vizuri hata kama ni dhahania.

## 2.3 Mapitio ya kazi Tangulizi

Sehemu hii inawasilisha mawazo makuu yatokanayo na mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusu ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Sababu ya kupitia maandiko mbalimbali ni kutokana na ukweli kwamba, utafiti umefanyika katika msingi wa tafiti zilizotangulia na kwamba maandiko yaliyotangulia kuhusu changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha yanasaidia kujua nini kimefanywa na nini hakijafanywa na watafiti waliotangulia.

Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha umetafitiwa na watafiti mbalimbali. Criper na Dodd (1984) walifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari,katika utafiti huo wataalamu hao walichunguza ujuzi wa lugha Kiingereza walionao walimu na wanafunzi katika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari nchini Tanzania. Ili kupata matokeo ya kile walichokuwa wakikichunguza,wataalamu hao walitoa majaribio kwa wanafunzi elfu mia nne na kumi kutoka ngazi yote za elimu. Matokeo ya majaribio hayo yaliwafanya wataalamu hao kugundua kuwa matumizi ya lugha ya Kiingereza kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari siyo njia sahihi ya kutolea elimu katika ngazi hizo.

Kueleweka kwa lugha ya Kiingereza kuko chini sana takribani katika shule zote zilizofanyiwa utafiti huo. Ni dhahiri kwamba matumizi ya Kiingereza yanafanya kujifunza kuwa kugumu. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa asilimia kumi ya wanafunzi wa kidato cha nne waliofanyiwa utafiti walikuwa na uwezo mdogo wa kuelewa kitu chochote kilichofundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Hali inaonyesha dhahiri ni changamoto katika ufundishji na ujifunzaji wa lugha ya kiingereza kwa wanafunzi wa sekondari.

Moochi (2013) katika utafiti wake juu ya changamoto za ujifunzaji lugha katika shule ya Nyamira anaeleza kwamba idadi ya wanafunzi katika darasa la ujifunzaji ni changamoto kubwa inayoweza kumzuia mwalimu asieleweke kwa wanafunzi hivyo kusababisha matokeo mabaya ya mitihani ya taifa. Hoja hiyo iliungwa mkono na Fasold&Linton (2006) ambao wanafafanua kwamba matokeo ya somo la Kingereza katika shule ya sekondari Nyamira yalikuwa mabaya kwa sababu idadi ya wanafunzi

ilikuwa kubwa mno kuliko kiwango cha zana za kufundishia. Bamgbose (2000) alifanya utafiti wake juu ya sababu za wanafunzi kufanya vibaya katika somo la Kifaransa nchini Rwanda na alibaini kuwa upungufu wa nyenzo za ujifunzaji ni changamoto kubwa sana inayowakabili wanafunzi wa shule za sekondari. Pia Mackey (2006) alifanya utafiti ili kubaini sababu zilizosababisha wanafunzi washindwe kufaulu vizuri somo la Kingereza katika shule za sekondari katika county ya Nakuru nchini Kenya na kubaini kwamba mazingira duni ya kujifunzia na mpangilio mbovu wa silabasi ni vyanzo vikubwa vinavyochangia ufaulu duni wa wanafunzi.

Naye Qorro (2006) katika utafiti wake nchini Tanzania kuhusu matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia shule za sekondari, utafiti wake ulibaini kuwa wanafunzi wengi na walimu wao wana matatizo katika matumizi ya lugha hiyo. Wanafunzi wachache sana huweza kushiriki katika tendo la kujifunza huku walio wengi wakishindwa kushiriki. Kujifunza na kufundisha kunaweza kuwa na mafanikio pale Walimu na Wanafunzi wanapomudu kutumia lugha ya kufundishia kwa sababu ufundishaji ni mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi. Hii inaonekana kuwa ni changamoto mojawapo katika ufundishaji na ujifunzaji.

Njongu & Nganje (2006) walifanya utafiti kuhusu changamoto za ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za upili zilizoko Nairobi nchini Kenya na matokeo ya utafiti wao ulibaini kwamba matumizi ya kitabu kimoja cha kufundishia kwa muda mrefu hasa sehemu ya fasihi andishi husababisha wanafunzi wakisome Kiswahili kwa lengo la kufaulu mtihani na si kutafuta ujuzi wa kuhakiki kazi za fasihi. Kwa hiyo lengo la kufaulu mtihani peke yake ni kikwazo kikubwa katika ujifunzaji wa

somo la Kiswahili nchini Kenya. Kwahiyo suala la zana za kufundishia katika somo la Kiswahili ni suala lisiloepukika kwa mwalimu kwani uongeza umilisi.

Mpemba (2007) alifanya utafiti kuhusu changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari mkoa wa Dar es Salaam na matokeo ya utafiti wake yalibainisha kwamba mbinu mbalimbali za kufundishia husaidia wanafunzi wawe na tabia ya udadisi. Yorandi (2013) alifanya utafiti kuhusu lugha ya kufundishia ya Kiswahili katika kufundisha na kujifunzia elimu shule za sekondari na vyuo vya ualimu. Katika utafiti huo, mtafiti alifanya majaribio ya kufundisha somo la Biolojia kwa wanafunzi wa kidato cha 1, 2 na 3 kwa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa mada alizozichagua kisha akatoa mtihani au majaribio ya kuwapima wanafunzi hao.

Matokeo ya majaribio hayo yalionesha kuwa wanafunzi walijifunza na kuelewa vizuri zaidi na kufaulu mitihani ya somo hilo iliyotungwa kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo ilidhihirisha maudhui ya somo la Biolojia yalieleweka vizuri zaidi kwa kufundishwa kwa lugha ya Kiswahili kuliko kwa lugha ya Kiingereza. Matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuwa:

i. Kiswahili ndiyo lugha inayoeleweka vizuri zaidi katika kufundishia na kujifunzia elimu shukeni na vyuoni
ii. Wanafunzi wengi hawaelewi lugha ya Kiingereza inapotumiwa kama lugha ya kufundishia.

Kwahiyo matumizi ya Kiingereza yamekuwa changamoto kwa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la biolojia na huwafanya wanafunzi wasiweze kupata elimu

ambayo wangeipata kwa manufaa ya kuliendeleza taifa. Ndio maana, UNESCO (1953) kwa upande wake inaona lugha za jamii ni bora katika kufundishia kuliko lugha zote za kigeni. Inabainisha sababu tatu kama ifuatavyo; moja, lugha ya jamii ni mfumo wa dhana zenye maana kwao ambazo katika akili ya mwanafunzi hufanya kazi haraka katika kujielezeka na kueleweka. Mbili, lugha ya mtu ni njia ya kujinasibisha na kwao; na tatu ni sababu ya kielimu ambayo kwa mwanafunzi hujifunza haraka kupitia lugha anayoielewa vema kuliko lugha ngeni.

Lugha mama humfanya kama ilivyosemwa hapo juu. Mwanafunzi ajifunze maarifa tu badala ya lugha ngeni na maarifa mageni. Hivyo somo la Kiswahili ni somo muhimu kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne na lugha ya Kiswahili ni muhimu kinatumika kila sehemu na hali hii ndiyo iliyofanya utafiti huu kuchunguza changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili

## 2.4 Kiunzi cha Nadharia

Sinclair (1995) anaeleza nadharia kama wazo au mfumo wa mawazo maalum unaolenga kufafanua suala fulani. Isitoshe, Pearshall na Trumble (1982) wanaeleza nadharia kuwa ni mfumo wa mawazo wa kuelewa jambo fulani; hasa ule ulio na misingi yake katika kanuni za kijumla zisizo na uhusiano na jambo linalofafanuliwa. Naye Massamba (2004) anadai kwamba, nadharia ni taratibu kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kuelezea jambo. Halikadhalika TUKI (2004) wanaunga mkono maana hiyo kwa kusema, nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani.

Ili mtafiti aweze kufanya utafiti wake kwa uthabiti na uamilifu, na utafiti huo uweze kuzaa matunda yanayotarajiwa ni lazima utafiti huo uongozwe na nadharia sahihi inayofaa kulingana na malengo ya utafiti huo. Hii ni kwa sababu nadharia ndiyo inayobeba mawazo au dhana au malengo yatolewayo kwa lengo la kuelezea hali na tukio fulani. Zipo nadharia mbalimbali zinazoelezea namna ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha iwe ya kwanza au lugha ya pili na baadhi ya nadharia za ujifunzaji wa lugha ni; Nadharia ya Utabia, Nadharia ya Uhulka, Nadharia Utambuzi, Nadharia ya Lugha mpito/Lugha Daraja na Nadharia ya Usasa Nyuzi Tofautishi.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Utabia. Nadharia hii iliasisiwa na John B. Watson mwaka 1913. Wengine wanaoshadadia nadharia hii ni Edward Thorndike 1935, Hull 1943 na kuimarishwa na Skinner 1957. Nadharia hii mwanzoni ilianza kwa kuzungumzia ujifunzaji na ujumla wake na baadae ikaonekana inafaa pia kwenye ufundishaji wa lugha. Kwa mujibu wa wanatabia ujifunzaji wa lugha ni mwigo kwa maana ya kwamba huiga kile kinachosemwa wanaomzunguka anayejifunza. Aliyetafiti zaidi katika nadharia ya ujifunzaji ni Skinner. Yeye anasema kuwa ujifunzaji wa lugha ni tabia na si suala la utambuzi wa akili na akasema kuwa kujifunza hutokea kwa kukariri. Mtoto hujifunza lugha kwa kuiga.

Kwa mujibu wa Skinner ujifunzaji wa lugha ni mwigo, Mtoto anaiga watu wazima wanapozungumza na katika kuiga huko mtoto husifiwa anapofanya vizuri, hurekebishwa au kuonywa na hujifunza kwa kurudiarudia. Aliimarisha Nadharia hii kwa kuongeza kuwa, mabadiliko ya uwezo wa tabia unatokana na michakato ya ujifunzaji na mazoea ya taaluma katika mazingira mahsusi. Watu wazima hujifunza

lugha kwa kuzingatia utamaduni wa jamii husika hivyo mazingira na utamaduni wake ndio nyenzo kuu inayomwezesha mtoto kuamilia lugha. Nadharia hii inatambua nafasi ya mazingira katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha. Kwake Skinner, matarajio ya kupata matokeo chanya katika somo humtia mwanafunzi hamasa ya kufaulu.

Kulingana na Thomdike (1935) na Skinner (1957), mihimili muhimu ya Nadharia ya Utabia katika ufundishaji ni kama ifuatavyo:

i. Kwa kuwa mtoto anajifunza lugha kwa kurudiarudia,basi mwalimu anatakiwa awe anafundisha kwa kurudiarudia na hata mwanafunzi aweze kurudiarudia kile anachofundishwa, kwa hiyo mwalimu atafundisha suala jipya kwa kukariri na kurudiarudia vipengele muhimu vya somo ili kuwawezesha wanafunzi kuelewa.

ii. Mtoto anapokosea arekebishwe na sio kumkatisha tamaa. Kwa hiyo mwalimu amwelekeze mwanafunzi vyema ili kutorudia makosa. Makosa ni kikwazo cha kujifunza. Makosa yapaswa kukatizwa na kuadhibiwa ili yasirudiwe tena. Makosa ni kikwazo cha kujifunza. Pia Mwalimu anatakiwa kuwa mfano bora kwa kile anachofundisha. Makosa haya ni kama athari ya lugha mama.

iii. Kuandika kufuate baada ya kusoma (kukariri  na kuzungumza) kwa sababu wanafunzi watakuwa wameelewa matumizi maalum ya lugha katika somo na kupata uzoefu tosha.

iv. Mazingira mazuri ya ujifunzaji wa mwanafunzi huchangia uelewa mzuri wa mwanafunzi/wanafunzi, kuwa jukumu la mwalimu ni muhimu sana  nalo ni

> kuongoza kila tukio darasani; kuwaelekeza wanafunzi kwa kutayarisha mazingira, kuteua mada inayofaa, kuandaa nyenzo za kufundishia. Jukumu la mwanafunzi ni kufuata maagizo. Hii ni safari ambayo mwalimu ataisafiri pamoja na wanafunzi wake.

Nadharia hii imetambua nafasi ya nyenzo katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili. Kulingana na Nadharia hii mwalimu hana budi kutumia nyenzo za ufundishaji ili kuweza kuimarisha matokeo chanya kwa wanafunzi wake wanaojifunza somo la Kiswahili. Nadharia ya Utabia inalenga kuelekeza namna tabia inavyojengwa. Hivyo matumizi ya nyenzo za ufundishaji katika somo la Kiswahili ni shughuli ambayo imependekezwa na wanasaikorojia wa Utabia. Nyenzo huwawezesha walimu kudhibiti hali, mihemko na uelewa wa wanafunzi wao. Hali hii husababisha mielekeo chanya dhidi ya wanafunzi wa somo la kiswahili. Nadharia hii inasisitiza kuwa nyenzo huimarisha uwezo wa mwanafunzi na humwezesha kuwa na kumbukumbu ya yale aliyofundishwa na mwalimu.

Vilevile Nadharia hii imepokea mabadiliko mbalimbali na maoni ya hivi karibuni zaidi ni ya Deodutus (2015) anaendelea kusisitiza kuwa kujifunza ni tukio la uhusiano wa matukio, mwitiko na kichocheo katika mazingira na uimarisho chanya au uimarisho hasi. Uimarisho chanya huhamasisha mwendelezo wa mwitiko wakati uimarisho hasi hufifisha au kuzuia mwitiko usiendelee. Deodutus (keshatajwa) anaona kuwa, mazingira yanatumika kwa maana pana zaidi kwa kuhusisha masuala ya ujifunzaji wa somo darasani. Madhumuni ya kukariri na kurudia yalikuwa ni kujaribu kujenge tabia inayofaa kuhusu somo na iliyo sahihi tabia au lugha isiyo na makosa kwani makosa yalionekana kama kikwazo cha kujenga tabia nzuri.

Kulingana na Deodutus, Nadharia hii ina umuhimu kwani; mwalimu ataweza kuwapatia wanafunzi mazoezi mwafaka, na wakati mwingine mazoezi hayo yataweza kurudiwarudiwa ili mwanafunzi aweze kuimarika katika somo. Nadharia ya Utabia inasisitiza mazoezi na utuzaji katika somo lolote. Walimu sawa na wanafunzi, wanatakiwa wafanye mazoezi mengi sana katika somo ili kuboresha utendaji na umilisi wao kama walimu. Mwisho kabisa, mwalimu ataweza kufundisha kwa kuzingatia mazingira bora darasani. Kulingana na nadharia hii mazingira mema husababisha ufundishaji bora na mabaya yakisababisha matokeo mabovu.

Hivyo katika Nadharia hii, ujifunzaji wowote wa somo ulionekana kama uamiliaji wa tabia mpya. Hali kadharika, ujifunzaji wa somo ni sawa na ujifunzaji mwingine wowote kutokana na kufanya mazoezi ya hiyo tabia mpya na kutoa marejesho sahihi. Naye Rodgers (1976) anasisitiza kuwa, Nadharia hii inawalenga walimu wa somo kutumia mbinu bora za ufundishaji wakishirikiana na wanafunzi wao. Schultz (1987), anaendelea kufafanua kwamba, walimu kutaka wanafunzi wajifunze vyema huibua msukumo unaowapa ufanisi huo. Kwa hiyo, walimu wa somo la Kiswahili yafaa waweze kuwa na nyenzo na kupanga mikakati wanayoitumia kufundisha ili kufikia malengo yao katika ufundishaji wa somo la Kiswahili.

Mtafiti amejiridhisha na kujitosheleza na kutumia Nadharia hii ya Utabia ya Skinner kama ilivyofafanuliwa hapo juu kwa sababu ina vigezo vya kutumia vyema katika utafiti huu, kwani Nadharia hii imetoa mwongozo fanisi kwa malengo na maswali yote ambayo yamejumuishwa katika utafiti huu. Nadharia ya Utabia inapendekeza walimu wahakikishe kuwa kuna vitabu vya marejeleo na kiada wanapofundisha masomo ikiwa ni pamoja na somo la Kiswahili. Mbunda (1976) analiunga mkono

suala hili kwa kuhakikisha kuna vitabu vya kiada katika vidato vya tatu na nne na kuwapa wanafunzi muda wa kutosha kujiandaa kwa mitihani. Kwa muhtasari, Nadharia hii ya Utabia imeongoza uchambuziwa malengo yote ya utafiti huu. Aidha Nadharia hii imejitosheleza katika kuchunguza matumizi ya nyenzo za kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunziwa somo la Kiswahili na pia kuchunguza maandalizi ya walimu kuhusu ufundishaji wa somo la Kiswahili.

## 2.5 Pengo la Utafiti

Kulingana na utalii wa kazi tangulizi, tumebaini kuwa suala la ufundishaji na ujifunzaji katika mfumo wa elimu Tanzania limeshughulikiwa kwa mitazamo, na kwa nyakati tofauti. Kwa mfano, Yorandi (2013) alifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia elimu ya shule za sekondari na vyuo vya ualimu, Pia Peterson (2006) alichunguza matumizi ya lugha ya asili ya Kafrika kama lugha ya kufundishia katika chuo kikuu kwa kuzingatia hoja ya kuanzishwa kwa idara ya Kiswahili.

Kwa jumla hakuna tafiti zilizokwisha fanyika katika wilaya ya Temeke zinazohusu changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili kwa shule za sekondari za Temeke. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu ulilenga kufanya uchunguzi wa changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa shule za sekondari wilaya ya Temeke kwa kuona matumizi ya nyenzo za kufundishia na upatikanaji wake, pia utafiti ulitathimini maoni ya walimu, wanafunzi na wakuu wa shule.

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii tumeona mapitio mbalimbali ya kazi tangulizi. Sura hi imeonesha mtazamo wa watalaam mbalimbali ulimwenguni kuhusiana na mada ya utafiti juu ya

lugha, ufundishaji, ujifunzaji na lugha ya kufundishia. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni utangulizi, inafuatiwa na sehemu ya pili ambayo ni mapitio ya kazi tangulizi, kiunzi cha nadharia na pengo la utafiti na sehemu ya mwisho ni hitimisho.

# SURA YA TATU

# MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imelezea kwa kina mbinu na njia ambazo zitatumika kufanya utafiti.Mtafiti ametumia vipengele mbalimbali kama vile usanifu na mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji na mbinu za ukusanyaji.

## 3.2 Usanifu na Mkabala wa Utafiti

Robson (2007) anaeleza uchunguzi kifani ni aina ya umbo la utafiti ambalo humpa mtafiti uhuru wa kuteua jambo moja mahususi ambalo atalichunguza kwa undani na kulitolea hitimisho muafaka. Vile vile uchunguzi kifani humuwezesha mtafiti kuelewa muktadha mzima wa jambo analolitafiti na hivyo kuwa rahisi kwake kukamilisha malengo ya utafiti wake. Kothari (2009) anafafanua mbinu ya uchunguzi kifani kuwa inamsaidia mtafiti kujibu maswali kama vile nini? kwa nini? kwa sababu gani? kivipi?, Good (1966) anasisitiza kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya utafiti kwa sababu ni ya uhakika inayomuwezesha mtafiti kupata taarifa muhimu na sahihi kwa kutumia muda na gharama ndogo. Utafiti huu ulijikita kutathimini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari wilaya ya Temeke. Mtafiti katika kufanikisha mada alitafiti walimu, wanafunzi na wakuu wa shule ili kuweza kufanikisha malengo ya utafiti wake.

Kuna mikabala mikuu miwili ya ukusanyaji na uwasilishaji wa data, mkabala wa kimaelezo na mkabala wa kitakwimu. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mikabala yote miwili. Mikabala hii ilitumika kwa sababu ilikidhi malengo yote ya utafiti.

Mkabala wa kimaelezo ambao data zake hupatikana kutoka kwa watafitiwa kisha zitachambuliwa kwa njia ya maelezo. Mkabala huu wa kimaelezo ulimsaidia mtafiti kwenda kukusanya data kwa watafitiwa kwa njia ya kutumia maswali yanayohusu mkabala huu wa kimaelezo. Kothari (1990), anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni njia ya kuchambua data katika muundo wa maelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu. Anasema ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Kwa mujibu wa Matinde (2014) takwimu ni njia mahsusi ya mawasiliano idhihirishayo kwa uwazi na uhakika chochote kile kinachohusika. Kwa hiyo data zilizokusanywa zilipangwa kwa takwimu na kufafanuliwa kwa njia ya maelezo ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wasomaji na mtafiti mwenyewe.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika wilaya ya Temeke ukijumuisha shule tano, shule mbili za sekondari zinazomilikiwa na serikali pamoja na shule tatu binafsi zilizopo katika kata ya Mibulani. Tuckman (1998) anasema kuwa wakati mwingine uzoefu wa eneo la utafiti humpa mtafiti kibali miongoni mwa wakazi wa eneo husika. Anatilia mkazo kuwa eneo linalofaa kwa utafiti ni lile linalofikiwa kwa urahisi na mtafiti na watafitiwa. Hivyo mtafiti alichagua eneo hili kwa sababu analielewa vyema. Pia mtafiti amechagua kufanya utafiti katika wilaya ya Temeke kwa sababu hajakumbana na utafiti wa aina hii ambao ulifanywa katika wilaya ya Temeke katika kuangazia changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari. Mtafiti alitarajia matokeo ya utafiti yataibua data halisi ambazo zitaweza kubainisha kinachotendeka katika sehemu nyingine nchini zenye sifa sawa

na eneo la wilaya ya Temeke.

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji

### 3.4.1 Kundi Lengwa

Kwa mujibu wa Peil (2002), si rahisi kuchunguza idadi nzima ya watu inayostahili kwani wakati na gharama ni vizingiti vikubwa. William (2011), anatolea maelezo juu ya maana ya kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti, yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Pia Kumar (2014) anaeleza kuwa walengwa wa utafiti ni watu ambao mtafiti amekusudia waweze kutoa taarifa kuhusu malengo ya utafiti.

Kwa ufupi, kundi lengwa ni jumla ya walengwa wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Katika utafiti huu kundi lengwa ilijumuisha walimu wa somo la Kiswahili waliokuwa wakifundisha kidato cha tatu, wanafunzi wa kidato cha tatu pamoja na wakuu wa shule za sekondari ambazo mtafiti alifanyia utafiti wake. Walengwa hawa walichaguliwa kwa sababu ndio wenye uwezo wa kutoa taarifa zinazohitajika kulingana na anuani ya utafiti huu ambao ulijikita kutathmini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

### 3.4.2 Sampuli ya Utafiti

Kwa mujibu wa Mligo (2012), sampuli ni kundi fulani la watu au vitu lililoko ndani ya mkusanyiko wa watu ambao mtafiti anaamini kwamba linalo habari zitakazomwezesha kujibu swali lake la utafiti. Pia Cohen (2007), amefafanua kuwa sampuli ni sehemu ndogo ya kundi kubwa na Creswell (2014), ameeleza kuwa sampuli ni sehemu ya kundi lengwa ambalo mtafiti anapanga kulisoma kwa ajili ya

kujumuisha kuhusu kundi kubwa. Hivyo kuchagua sampuli ni kuchagua kundi dogo la watu au vitu katika mkusanyiko wenye makundi ya aina nyingi kwa malengo maalumu aliyonayo mtafiti kwa ajili ya utafiti wake.

Kutokana na ufafanuzi huo, kwa kuzingatia muda na gharama za fedha ni vingumu kushirikisha shule zote za sekondari wilaya ya Temeke. Hivyo basi Kwa kuwa si rahisi kwa mtafiti kuwatafiti walimu, wanafunzi na wakuu wa shule wote wa wilaya ya Temeke kutoka kata ya Mibulani. Utafiti huu ulilenga sampuli ya watafitiwa wachache ambao walisaidia kujibu maswali yaliyolengwa kwenye utafiti huu ili kupata data. Kwa hiyo jumla ya watoa taarifa mia na ishirini (120) walihusika katika utafiti huu. Watoa taarifa hao ni wanafunzi mia moja (100) wa kidato cha tatu, walimu kumi na tano (15) wa somo la Kiswahili na wakuu wa shule watano (5) kutoka shule tano (5) za sekondari za serikali mbili (2) na binafsi tatu (3) ambazo mtafiti alifanya utafiti wake. Sababu ya kuteuliwa kwa wanafunzi wa kidato cha tatu ni kuwa wanafunzi hawa wamekuwa na miaka mitatu ya ujifunzaji na wana muda mzuri wa kutafitiwa. Kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza ni wageni, wanafunzi wa kidato cha pili na wanafunzi wa kidato cha nne hawa wanakabiliwa na majaribio na maandalizi ya mtihani wa taifa hivyo wasingefaa kufanyiwa utafiti kwa sababu wanabanwa na muda. Sampuli hii ilisaidia kupata majibu bora ya utafiti.

### 3.4.3 Usampulishaji wa Utafiti

Usampulishaji kama walivyoeleza Adam na Kamuzora (2008), ni mbinu, mchakato au kitendo cha kutafuta walengwa wa utafiti. Sign (2007) anaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Kwa mujibu wa Sharma (2017)

kuna aina kuu mbili za usampulishaji, nazo ni usampulishaji usionasibu na usampulishaji nasibu. Usampulishaji nasibu ni aina ya usampulishaji ambao kila mtafiti ana fursa sawa ya kushiriki katika utafiti. Aina hii ya usampulishaji hujumuisha usampulishaji nasibu sahili, usampulishaji nasibu taratibishi na usampulishaji nasibu tabatishi.

Usampulishaji usionasibu ni aina ya usampulishaji ambao hautoi fursa sawa kwa watafitiwa kushiriki katika utafiti. Aina hii ya usampulishaji hujumuisha usampulishaji usionasibu legwa (kusudio), usampulishaji usionasibu tajwa na usampulishaji usionasibu fursa, Kothari (2004). Sharma (keshatajwa) anaeleza kuwa, usampulishaji usionasibu kusudio na usampulishaji usionasibu fursa ni njia ya kupata sampuli ya utafiti ambayo mtafiti huichagua huku akiwa na matarajio kuwa itawakilisha kundi lengwa. Hata hivyo, mchakato wa usampulishaji sio kazi rahisi hasa katika mchakato wa uteuzi wa shule kwa sababu ya uwepo wa shule nyingi zilizopo katika wilaya ya Temeke. Kutoka na chngamoto hiyo Gorter (2016) anashauri kuwa ni vizuri matafiti kujiwekea mipaka.

Hivyo basi, katika utafiti mbinu ya usampulishaji usinasibu kusudio na usampulishaji usionasibu fursa zilitumika katika kuteua sampuli ya utafiti huu. Sababu ya kutumia usampulishaji usionasibu kusudio ni kwaamba sio rahisi kuchunguza shule zote za sekondari wilaya ya Temeke. Shule ziliteuliwa kwa misingi ya matabaka mawili, shule za binafsi tatu (3) na shule za serikali (2) jumla ni shule tano (5) kutoka kata ya Mibulani ambazo mtafiti alichagua. Aidha, usampulishaji usinasibu fursa ulitumika katika sampuli ya utafiti huu kwa sababu mchakato wa kukusanya data za utafiti ulitegemea wanafunzi ishirini (20) kutoka

shule tano na kuwa na sampuli ya wanafunzi wa kidato cha tatu mia moja (100), walimu wa kuu watano (5) kwa idadi ya mmoja mmoja kutoka kila shule na walimu wa somo la Kiswahili wa tatu (3) kutoka sule tano na kuwa na jumla ya walimu kumi na tano (15). Sababu ya kuteua shule tano ambazo zilitoa wanafunzi wa kidato cha tatu mia moja (100), walimu wa somo la Kiswahili kumi na tano (15) na wakuu wa shule watano (5) ni ilionekana kuwa idadi hii inatosha kutoa taarifa za kuaminika kuhusu utafiti huu, pia kulingana na upana wa eneo la utafiti kijiografia, haikuwa rahisi kutafiti shule zote katika wilaya ya Temeke. Njia hii ilitoa mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa taarifa.

### 3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Kothari (2004), ukusanyaji wa data ni zoezi la awali ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa ambazo yeye amezikusudia ili kufanikisha malengo aliyoyakusudia. Data za utafiti huu zimekusanywa kutoka maktabani na uwandani. Kothari (ameshatajwa) anasema data za upili (maktabani) ni zile ambazo tayari zilikusanywa na zimeshatumika na zimehifadhiwa. Mtafiti alitumia njia hii kupata data na amezipata kupitia maandiko ya wataalamu mbalimbali pamoja na ripoti za aina mbalimbali kwa kutumia mbinu ya usomaji maandiko.

Taarifa hizo zimekusanywa kwa kuangalia kazi zilizopita kuhusiana na mada kwa kuangalia vitabu, majarida, machapisho na tafiti mbalimbali katika maktaba ya Chuo Huria cha Tanzania tawi la Dar es salaam-Kinondoni. Data za msingi (uwandani) kama anavyozielezea Kothari (ameshatajwa) ni zile data ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza uwandani. Data hizi zimekusanywa wakati mtafiti yupo uwandani katika kata ya Mibulani. Data hizo ndizo zimejibu maswali ya utafiti, data za

uwandani zimekusanywa kwa kutumia mbinu mbili za ukusanyaji data: Mbinu hizo ni hojaji na mahojiano,

### 3.5.1 Hojaji

Kwa mujibu wa Kothari (2014), hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandaa maswali au dodoso yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Mbinu hii ni ya kutumia maswali yaliyoandikwa kwa lengo la kujibiwa na mtafitiwa. Aidha, Mligo (2012), anaendelea kudai kwamba, hojaji ni karatasi iliyoandikwa maswali ambayo hupewa mtafitiwa ili aandike majibu. Kulingana na maelezo ya wataam hao,hojaji ni maswali yatakayoandikwa na mtafiti kwa lengo la kumhoji mtafitiwa na maswali haya yatafungamana na malengo ya utafiti husika, data hukusanywa kutokana na mtafitiwa kujibu maswali yaliyoorodheshwa katika karatasi.

Kwa mijibu wa William (2011), kuna maswali ya hojaji ya aina mbili. Aina ya kwanza, ni maswali funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jawabu. Aina hii ni rahisi kujibu na kuchanganua. Pia, inasaidia kupata majibu mahususi na huepusha upendeleo. Aina ya pili ya maswali ya hojaji yasiyo funge yaani maswali wazi ambayo yatahitaji maoni, maelezo na mitazamo ya wasailiwa, kwahiyo yatatoa hutoa fursa au uhuru kwa watafitiwa kueleza wanachokijua na kumsaidia mtafiti kupata taarifa nyingi zaidi.

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu hii katika kukusanya data kuhusu nyenzo za kufundishia na kujifunzia wa somo la Kiswahili, maandalizi ya walimu na maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Hojaji ilikuwa ya muhimu katika utafiti kwa sababu ilisaidia katika kuchunguza

changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Hojaji zilizotumiwa zilikuwa na maswali ya aina zote mbili yaani maswali funge na wazi kama inavyopendekezwa na Wamitila (2004). Sehemu funge ilikuwa na maswali na majibu ambapo mtafitiwa alihitajika kuchagua jibu kisha kulikuwa na maswali wazi ambayo yalihitaji maoni, maelezo na mitazamo ya watafitiwa. Utafiti huu ulikuwa na hojaji mbili, hojaji ya mwalimu ambayo ilikuwa imegawanyika katika sehemu nne na hojaji ya mwanafunzi ambayo ilikuwa imegawanyika katika sehemu tatu. Hojaji zote ziliandaliwa ipasavyo katika kukidhi malengo na maswali ya utafiti.

### 3.5.2 Mbinu ya Usaili

Hii ni mbinu ambayo mtafiti anakusanya data akiwa ana kwa ana na mtafitiwa. Enon (1998), anafasili kuwa ni mbinu ya kuuliza maswali ya ana kwa ana, simu au barua pepe kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu swali la utafiti lililoainishwa. Kothari (2014), anasema kuwa, njia hii hutumika kukusanya data na huwasilishwa kwa njia ya mdomo ana kwa ana baina ya mtafiti na mtafitiwa. Mtafiti ataweza kufafanua masuala ambayo hayaeleweki kwa mtafitiwa. Hali kadhalika mtafitiwa atapata nafasi ya kufafanua majibu au kumtaka mtafiti kuliweka wazi swali ambalo halitaeleweka ipasavyo kwa mtafitiwa. Kwa hiyo mahojiano ni mbinu inayohusisha kujieleza kwa mdomo katika kuuliza na kujibu maswali.

Katika utafiti huu mbinu hii pia ilitumika. Ili kuhakikisha kuwa data halisi zinapatikana, usaili ulikwepa upendeleo, sampuli ilihojiwa kwa kufuata mpangilio sawa maswali yaliyosomwa jinsi yalivyokuwa yameandikwa na maswali hayo yaliulizwa bila kuonyesha kuwa yalimlenga mhojiwa binafsi. Vilevile maswali

yalirudiwa kila ilipohitajika, Grey (2004). Majibu yaliandikwa jinsi yalivyotolewa na wahojiwa bila kuongezea hisia za mtafiti. Utafiti huu ulikuwa na maswali ya usaili ya aina mbili, aina ya kwanza ni maswali ya usaili kwa walimu wa somo la Kiswahili na aina ya pili ni maswali ya usaili kwa wakuu wa shule.

**3.6 Hitimisho**

Sura hii imechambua mbinu za utafiti, eneo la utafiti limetajwa kuwa ni katika wilaya ya Temeke, sampuli na usampulishaji ukijumuisha walengwa wa utafiti ambao ni waalimu, wanafunzi na wakuu wa shule, njia ya mahojiano na hojaji zimeelezwa kuwa zilitumika katika kukusanya data za utafiti

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusika na umewasilishajina uchambuzi wa data zilizopatikana uwandani juu ya changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia misingi na kanuni za kiunzi cha Nadharia ya Utabia ya Skinner (1957) na kuimarishwa Deodutus (2015). Data zote ziliwasilishwa kulingana na malengo ya utafiti na maswali yake. Data hizi zilichanganuliwa kwa mtindo wa maelezo na takwimu, maelezo yalitolewa kwa ufupi yakiambanishwa na majedwali yenye takwimu ili kurahisisha usomaji wa maudhui yatokanayo na uchambuzi.

## 4.2 Changamoto za Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundishia

Lengo la sehemu hii ilikuwa ni kutafuta majibu kwa lengo la kwanza ambalo lilikuwa ni kuthamini changamoto za upatikanaji wa nyenzo za kufundishia kwa walimu wa somo la Kiswahili. Nyenzo katika ufundishaji wa somo la Kiswahili ni muhimu. Nyenzo hizi zinapotumiwa vilivyo huwafanya wanafunzi kuelewa wanachofundishwa na kuvutiwa na somo. Sehemu hii ina sehemu ndogondogo kulingana na maswali ya hojaji na mahojianoyaliyofanyika kwa walimu kumi na tano wa somo la Kiswahili.

### 4.2.1 Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundishia

Upatikanaji wa nyenzo hufanikisha ufundishaji na urahisisha kazi kwa mwalimu katika ufundishaji. Mtafiti alitaka kubaini nyenzo zinazopatikana shuleni. Utafiti ulifichua kwamba shule nyingi zilikosa nyenzo za kufundishia somo la Kiswahili

kwa viwango tofauti. Utafiti ulibaini kuwa baadhi ya nyenzo ambazo zinaweza kuimarisha ufundishaji hazipatikani hata zikipatikana bado hazitoshelezi mahitaji. Katika kubaini hilo mtafiti aliwashirikisha watafitiwa katika maswali ya hojaji na usaili. Katika maswali ya hojaji, watafitiwa walipewa nafasi ya kuamua upatikanaji wa nyenzo shuleni kwa kuamua ipo, haipo, ipo lakini haitoshi au ipo lakini haitumiki kwa kuweka tiki kwa nyenzo zilizoorozeshwa na mtafiti. Matokeo yanaoneshwa katika jedwali Na.4.1.

**Jedwali 4.1 Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundishia**

| Nyenzo | Ipo | Haipo | Ipo lakini haitoshi | Ipo lakini haitumiki | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | 4 (26.7%) | 0 (0%) | 11 (73.3%) | 0 (0%) | 15 (100%) |
| Vitabu vya ziada/ marejeleo | 2 (13.3%) | 5(33.3%) | 8 (53.3%) | 0 (0%) | 15 (100%) |
| Miongozo ya walimu | 10 (66.7%) | 0 (0%) | 5 (33.3%) | 0 (0)% | 15 (100%) |
| Silabasi | 10 (66.7%) | 0 (0%) | 5 (33.3%) | 0 (0%) | 15 (100%) |
| Kamusi | 3 (20%) | 6 (40%) | 3 (20%)) | 3 (20%) | 15 (100%) |
| Maktaba | 3 (20%) | 9 (60%) | 0 (0%) | 3 (20%) | 15 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Matokeo katika jedwali 4.1 yanaonyesha, jumla ya watafitiwa wote waliohusika kwenye hojaji walikuwa kumi na tano sawa na asilimia mia moja (100%). Watafitiwa wote kumi na tano, walihusika katika kuamua upatikanaji wa vitabu vya kiada shuleni. Walimu 10 (66.7%) walikubali kuwa vitabu vya kiada vipo lakini haitoshi, na walimu 4 (26.7%) walisema vitabu vya kiada vipo. Pia katika upatikanaji wa vitabu vya ziada walimu 8 (53.3%) waliamua vipo lakini havitoshi, walimu 5 (33.3%) waliamua haipo na 2 (13.3%) waliamua vitabu vya ziada vipo.

Upatikanaji wa miongozo ya walimu na silabasi maamuzi yalifanana kwani, wahojiwa 10 (66.7) walionesha kuwa ipo na 5 (33.3%) walisema ipo lakini haitoshi. Kwa upande wa upatikanaji wa kamusi, walimu 6 (40%) walisema kamusi hazipo, 3 (20%) kamusi waliamua zipo, 3 (20%) waliamua kamusi zipo lakini hazitoshi na 3(20%) waliamua zipo lakini hazitumiki. Vilevile kwa upande wa maktaba, watafitiwa 3 (20%) walisema ipo, watafitiwa 9 (60%) walisema haipo na 3 (20%) walikiriipo lakini haitumiki.

Katika maswali ya mahojiano mtafiti alitaka watafitiwa kutaja nyenzo zinazopatikana shuleni na kubainisha iwapo kuna changamoto katika upatikanaji wa nyenzo na kama nyenzo hizo zinatosheleza ufundishaji. Watafitiwa wote 15 (100%) walibainisha kwambanyenzo zinazopatikana ni vitabu vya kiada, vitabu vya ziada, silabasi, kamusi na maktaba lakini kuna changamoto katika upatikanaji wake kwani baadhi ya nyenzo ni ghali. Maktaba hutumia gharama kubwa kuakikishaupatikanaji wake. Pia vitabu vya kiada, ziada, kamusi na silabasi ni vichache kulinganisha na idadi ya walimu hivyo husababisha changamato katika matumizi yake hali inayosabaisha uhaba wa nyenzo.

Savignon (2005) anadai kuwa, uwepo wa nyenzo za kufundishia hutekeleza jukumu kubwa katika kufanikisha ufundishaji wa somo la lugha. Kwa matokeo haya ni dhahiri kwamba suala la upatikanaji wa nyenzo kama sehemu ya kuimarisha ufundishaji bado ni changamoto. Ufundishaji bora unajengwa na upatikanaji wa nyenzo hivyo kama nyenzo zilizotajwa zinakosekana katika shule nyingi ambazo mtafiti alizitafiti matokeo mazuri ambayo walimu huyategemea itakuwa ni changamoto kuyapata.

### 4.2.2 Sababu Zinazoathiri Uteuzi wa Nyenzo za Kufundishia Somo la Kiswahili

Ili kufanikisha ufundishaji wa Kiswahili katika shule za sekondari, mwalimu hana budi kutumia nyenzo za kufundishia. Katika maswali ya hojaji mtafiti alitaka kujua sababu au vigezo gani vinavyoathiri uteuzi wa matumizi ya nyenzo za kufundishia somo la Kiswahili. Watafitiwa jumla yao walikuwa kumi na tano-wanaume sita ma wanawake tisa. Matokeo yalikuwa kama inavyojithihirisha katika jedwali Na.4.2.

**Jedwali 4.2 Sababu Zinazoathiri Uteuzi wa Matumizi ya Nyenzo katika Ufundishaji wa Somo la Kiswahili**

| Kauli | Ndiyo | Hapana | Jumla |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 10 (66.7%) | 5 (33.3%) | 15 (100%) |
| **Urefu wa mada** | 7 (46.7%) | 8 (53.3%) | 15 (100%) |
| **Ushiriki mdogo wa wanafunzi** | 6 (40%) | 9 (60%) | 15 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Watafitiwa jumla yao walikuwa 15 (100%). Matokeo yanaonyesha walimu 10 (66.7%) walisema idadi kubwa ya wanafunzi inathibiti au kuathiri uteuzi wa matumiziya nyenzo katika ufundishaji wa somo la Kiswahili na 5 (33.3%) wao walisema suala la idadi ya wanafunzi sio kugezo cha uteuzi wa nyenzo za kufundishia. Pia watafitiwa 7 (46.7%) waliafiki kuwa urefu wa mada huathiri uteuzi wa matumizi ya nyenzo na 8 (53.3%) walisema hapana. Katika suala la ushiriki mdogo wa wanafunzi, matokeo yanaonesha walimu 6 (40%) hukubana na kigezo hiki wakati 9(60%) wao walijibu hapana. Matumizi ya nyenzo ni muhimu katika ufundishaji ingawa walimu hukumbana na vikwanzo ambavyo hufanya uteuzi wa nyenzo kuwa changamoto. Ni nyema vikwazo hivi vikatatuliwa ili kumsaidia mwalimu kutumia nyenzo bila kupuuza.

### 4.2.3 Idadi ya Matumizi ya Nyenzo za Kufundishia

Katika maswali ya hojaji, mtafiti aliwataka watafitiwa kukadiria ni mara ngapi hutumia nyenzo katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Hivyo mtafiti alitaka kujua mara-idadi ya kutumia nyenzo za kufundishia somo la Kiswahili kwa kuweka tiki panapofaa. Jedwali Na.4.3 linaonesha taarifa hizo.

**Jedwali 4.3 Idadi ya Matumizi Ya Nyenzo Za Kufundishia**

| **Nyenzo** | **Mara kwa mara** | **Mara chache** | **Haitumiki kabisa** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | 15 (100%) | 0 (0%) | 0 (0%) | 15 (100%) |
| Vitabu vya ziada | 10 (66.7%) | 5 (33.3%) | 0 (0%) | 15 (100%) |
| Miongozo ya walimu | 15 (100%) | 0 (0%) | 0 (0%) | 15 (100%) |
| Silabasi | 15 (100%) | 0 (0%) | 0 (0%) | 15 (100%) |
| Kamusi | 6 (40%) | 9 (60%) | 0 (0%) | 15 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Matokeo yameonyeshwa kuwa walimu 15 (100%) hupenda kutumia vitabu vya kiada katika kufundishia mara kwa mara. Pia matumizi ya vitabu vya ziada, walimu 10 (66.7%) hutumia mara kwa mara katika ufundishaji, walimu 5 (33.3%) matumizi yao ni ya mara chache. Katika matumizi ya silabasi na miongozo ya walimu, walimu hutumia mara kwa mara katika ufundishaji hivyo walimu 15 (100%) wanatumia nyenzo hizi. Matokeo yalionyesha walimu 6 (40%) hutumia kamusi mara kwa mara, walimu 9 (60%) hutumia mara chache.

Matokeo haya yanashadidia ukweli kwamba ingawa kuna uhaba wa nyenzo za kufundishia lakini walimu wanaonyesha jitihada za kutumia nyenzo za kufundishia. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Dales (1999) anapodai kuwa nyenzo za kufundishia humpa mwanafunzi uwezo zaidi. Kutokana na matokeo ya utafiti ni

muhimu kuendelea kutilia mkazo matumizi ya nyenzo mara kwa mara kwa manufaa ya walimu na wanafunzi. Kwa kuwa uhaba wa nyenzo husababisha wanafunzi kupunguza morali ya matumizi ya nyenzo katika ujifunzaji,

### 4.3 Upatikanaji na Kiwango Cha Matumizi ya Nyenzo za Kujifunzia

Sehemu hii ilizingatia kujibu lengo la pili linalosema kuchunguza changamoto za upatikanaji na matumzi ya nyenzo za kujifunzia kwa wanafunzi wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Lengo liligawanyika katika sehemu ndogondogo ili kuweza kutoa taarifa za kina juu ya lengo hilo. Mtafiti alitaka kujua upatikanaji wa nyenzo za kujifunzia somo la Kiswahii na namna ambavyo nyenzo hizo hutumiwa katika ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

#### 4.3.1 Upatikanaji wa Nyenzo za Kujifunzia

Utafiti ulitaka kuchunguza upatikanaji wa nyenzo za kujifunzia kwa wanafunzi wa somo la Kiswahili. Katika maswali ya hojaji watafitiwa walipatanafasi ya kuamua iwapo nyenzo zipo, hazipo, zipo lakini hazitoshi na zipo lakini hazitumiki. Matokeo haya yanajithihirisha katika jedwali Na. 4.4.

**Jedwali 4.4 Upatikaji wa Nyenzo za Kujifunzia**

| Nyenzo | Ipo | Haipo | Ipo lakini haitoshi | Ipo lakini hatumiki | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | 15 (15%) | 10 (10%) | 60 (60%) | 15 (15%) | 100 (100%) |
| Vitabu vya ziada/ marejeleo | 15 (15%) | 55 (55%) | 20 (20%) | 10 (10%) | 100 (100%) |
| Kamusi | 10 (10%) | 50 (50%) | 10 (10%) | 30 (30%) | 100 (100%) |
| Maktaba | 20 (20%) | 40 (40%) | 0 (0%) | 40 (40%) | 100 (100%) |
| Michoro | 20 (20%) | 80 (80%) | 0 (0%) | 0 (0%) | 100 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Kutokana na matokeo ya jedwali na.4.4, imebainika kuwa, wanafunzi 60 (60%) walisema vitabu vya kiada vipo lakini havitoshi, wanafunzi 15 (15%) walisema vitabu vya kiada vipo, 15 (15%) walisema vipo na idadi ya wanafunzi 10 (10%) walisema havipo. Pia data zinaonyesha upatikanaji wa vitabu vya ziada ni 15 (15%) na idadi wa wanafunzi 55 (55%) wanadhihirisha hakuna vitabu vya ziada shuleni. Aidha wanafunzi 20 (20%) walijibu kuwa vitabu vya ziada vipo lakini havitoshi na wanafunzi 10 (10%) walisema vipo lakini havitumiki.

Kuhusiana na upatikanaji wa kamusi, wanafunzi 10 (10%) walisema zipo, na idadi ya wanafunzi 50 (50%) wanadhihirisha hakuna kamusi sheleni, 10 (10%) ipo lakini havitoshi na 30 (30%) walisema kamusi zipo lakini havitumiki. Vilevie Upatikanaji wa maktaba ni wanafunzi 20 (20%) wanadhihirisha maktaba ipo shuleni, wanafunzi 40 (40%) walisema hakuna maktaba na 40 (40%) walidhihirisha maktaba ipo lakini haitumiki. Upatikanaji wa michoro, idadi ya watafitiwa 20 (20%) walisema ipo na wafatifiwa 80 (80%) walidhibitisha hakuna michoro. Nyakomba (2002) anatoa kauli kwamba ni vyema kutumia nyenzo na kuzielewa.

Ujifunzaji wa somo la Kiswahili unahitaji kuwapo kwa nyenzo za kujifunzia ili kuongeza umakini na uelewa wa mwanafunzi. Ni dhahiri kuwa shule zinahitaji mikakati mwafaka katika kuhakikisha nyenzo za kujifunzia zinapatikana ili kuongeza morali kwa wanafunzi kupenda somo la Kiswahili. Utafiti umedhihirisha kuwepo na upungufu wa nyenzo za kujifunzia somo la Kiswahili kwani baadhi ya nyenzo zipo lakini bado hazitoshelezi idadi.

### 4.3.2 Kiwango cha Matumizi ya Nyenzo za Kujifunzia

Ili kufanikisha ujifunzaji wa somo la Kiswahili, wanafunzi hawana budi kuwa na

mazoea ya utumiaji wa nyenzo. Kwa kutumia hojaji, mtafiti alitaka kufahamu viwango vya matumizi ya nyenzo za kujisomea somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa somo la Kiswahili. Viwango hivi vilipimwa na mazoea ya utumiaji wa nyenzo. Watafitiwa 100 katika hojaji wanaosoma somo la Kiswahili waliweza kutoa maoni kama yanavyooneshwa katika jedwalina.4.5

**Jedwali 4.5: Matumizi ya Nyenzo Katika Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili**

| **Nyenzo** | **Mara kwa mara** | **Mara chache** | **Haitumiki kabisa** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | 15 (15%) | 70 (70%) | 15 (15%) | 100 (100%) |
| Vitabu vya ziada/ marejeleo | 20 (20%) | 30 (30%) | 50 (50%) | 100 (100%) |
| Silabasi | 0 (0%) | 10 (10%) | 90 (90%) | 100 (100%) |
| Kamusi | 10 (10%) | 10 (10%) | 80 (80%) | 100 (100%) |
| Maktaba | 5 (5%) | 15 (15%) | 80 (80%) | 100 (100%) |
| Michoro | 5 (5%) | 15 (15%) | 80 (80%) | 100 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Viwango vya matumizi ya nyenzo za kujifunzia yanaonyesha kuwa, wanafunzi 70 (70%) ni mara chache hupenda kutumia vitabu vya kiada, wanafunzi 15 (15%) wao ni mara kwa mara hutumia vitabu vya kiada na wanafunzi15 (15%) wao hawatumi kabisa vitabu vya kiada. Utafiti uliendelea kupata data za matumizi ya vitabu vya ziada na matokeo yalijidhihirisha kuwa 50 (50%) hawatumi kabisa vitabu vya ziada, watafitiwa 30 (30%) hutumia marachache na watafitiwa 20 (20%) hutumia vitabu vya ziada mara kwa mara. Utafiti ulibaini kuwa, wanafunzi 90 (90%) hawana matumizi ya silabasi na wanafunzi 10 (10%) ndio hutumia mara chache silabasi.

Utafiti ulionyesha kuwa matumizi ya kamusi ni 10 (10%) hutumiwa mara kwa mara, wanafunzi 10 (10%) hutumiwa mara chache na 80 (80%) haitumiki kabisa. Matumizi ya maktaba, data zinaonyesha wanafunzi 80 (80%) hawatumi kabisa, wanafunzi 15 (15%) hutumia mara chache na watafitiwa 5 (5%) hutumia mara kwa mara maktaba kama nyenzo ya kujisomea. Matumizi ya michoro, wanafunzi 5 (5%) hutumia mara kwa mara, wanafunzi 15 (15%) hutumia mara chache na wanafunzi 80 (80%) hawatumi kabisa. Brown (1993) anasisitiza kuwa, matumizi ya nyenzo za kujifunzia huchochea shauku na kumpa mwanafunzi morali ya kushiriki katika kipindi.

Matumizi ya kila nyenzo za kujifunzia ni suala muhimu katika kuongeza morali ya wanafunzi kuelewa somo. Lakini matokeo yanadhihirisha kuwa baadhi ya nyenzo ambazo hazitumiki kwa kiwango kikubwa kama vile maktaba, kwani 80 (80%) hawatumi kabisa kama nyenzo ya kujifunzia. Hivyo ni dhahiri walimu wana kazi ya kurudisha morali ya wanafunzi kupenda kutumia nyenzo hii mara kwa mara kama sehemu ya kuimarisha ufaulu wa wanafunzi kwa sababu wataimarisha morali ya kupenda somo. Savignon (2005) anadai kuwa, uwepo wa nyenzo za kufundishia hutekeleza jukumu kubwa katika kufanikisha ufundishaji wa somo la lugha.Naye Brown (1993) anasisitiza kuwa, matumizi ya nyenzo za kujifunzia huchochea shauku na kumpa mwanafunzi morali ya kushiriki katika kipindi. Kwa matokeo haya ni dhahiri kwamba suala la matumizi ya nyenzo kama sehemu ya kuimarisha ufundishaji linatakiwa kutiliwa msisitizo.

### 4.4 Maandalizi katika Ufundishaji

Sehemu hii inashughulikia lengo la tatu ambalo ni maandalizi ya walimu. Sehemu

hii imegawanyika katika sehemu sita, ambazo zimetoa matokeo yenye kujibu swali na lengo letu la tatu kulingana na maswali ya hojaji na usaili. Kufanikiwa kwa mpango wowote kunahitaji maandalizi bora ya mapema. Maandalizi hupanua uwezo wa mwalimu wa kuitafsiri silabasi na kuwa na muongozi mzuri wa ufundishaji darasani. Ilikuwa ni muhimu kwa utafiti huu kujua maandalizi ya mwalimu wakati wa ufundishaji ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

### 4.4.1Maandalizi Kabla ya Kuingia Darasani

Mtafiti alitumia hojaji katika kubaini iwapo walimu hujiandaa kabla a kuingia darasani. Matokeo yanaonyesha kuwa watafitiwa wote 15 (100%) hujiandaa kabla ya kufundisha somo la Kiswahili. Matokeo haya yanaungwa mkono na Odera (2010) anasisitiza kuwa, mwalimu mwenye uwezo ni yule anayefanya maandalizi ya kina kabla ya kungia darasani. Lewis na Hill (1985) wanasisitiza kuwa maandalizi ya kina ni sharti yafanywe na mwalimu kabla ya kuingia darasani. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yanadhihirisha kuwa walimu wengi wanajiandaa kabla ya kuingia darasani. Hali hii inaonyesha ubora wa walimu katika maandalizi.

### 4.4.2 Mahudhurio ya Semina au Warsha Juu ya Ufundishaji

Ilikuwa ni muhimu kujua maandalizi ambayo walimu hufanya na hufanyiwa na shuleni kama sehemu ya kuongeza ufanisi zaidi katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Baada ya walimu kumaliza chuo cha elimu, je hupata mafunzo ya kuwapiga msasa katika uimarisha na kuendana na mabadiliko ya ufundishaji duniani? Katika kupata data, walimu 15 walijibu maswali ya hojaji na kufanyiwa usaili ili kuweza kupata matokeo. Matokeo ya hojaji yanadhihirishwa katika Jedwali na.4.6.

**Jedwali 4.6 Mahudhurio ya Semina au Warsha**

| **Mahudhurio ya semina au warsha** | **Ndiyo** | **Hapana** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Asilimia ya waliohudhuria | 4 (26.7%) | 11 (73.3%) | 15 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Matokeo yanafichua kuwa walimu 4 (26.7%) waliwai kuhudhuria semina au warsha za ufundishaji nawalimu 11 (73.30%) wamejibu kuwa hawajawai kuhudhuria semina za ufundishaji. Pia kwa kutumia mahojiano, mtafiti aliomba kujua kama walimu wamewahi kuhudhuria semina au warsha za kuendeleza ujuzi. Walimu 4 (26.7%) walisema waliwahi kuhudhuria semina lakini ni mara moja tu. Aidha walimu 11 (73.3%) wao walijibu hawajawahi kuhudhuria semina au warsha za kuimarisha ufundishaji wa somo la Kiswahili. Muruguru (2000) anashauri kuwa kozi za kupiga msasa huwa nzuri kwa kujaza pengo pale walimu wanapogundua upungufu wowote, Maoni yake yanaungwa mkono na Killen (2006) ambaye anashauri kuwa taaluma zote, ikiwemo ualimu humhitaji mtaaluma kuyaimarisha masomo yake wakati wote atakaokuwa akifanya kazi ilia pate maarifa na ujuzi mpya wa kuimarisha umilisi wake, hususani kwenye ufundishaji.

Hali hii inaonyesha udhaifu katika maandalizi ya walimu na kudhihirisha kuwa kuna changamoto. Hivyo taasisi na wizira ya elimu zinatakiwa kuwajibika katika kuakikisha warsha au semina wezeshi katika ufundishaji zinaimarishwa kwa sababu mafunzo husaidia kuimarisha na kuendeleza morali katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Pia mafunzo huwasaidia walimu kupata maarifa mapya ili kuweza kuziba pengo katika upungufu wowote na kuvuta kumbukumbu kwa yale yaliyosahulika.

### 4.4.3 Idadi ya Mahudhurio Semina au Warsha

Katika sehemu hii, walimu 15 (15%) wa somo la Kiswahili walitafitiwa. Walimu hawa (wanawake na wanaume) wanatofautiana katika uzoefu wa kufundisha Kiswahili kutokana na utofauti wa uelewa wanaojengewa kwenye semina elekezi za somo la Kiswahili. Kama inayojidhihirisha katika jedwali na. 4.7

**Jedwali 4.7: Idadi ya Mahudhurio ya Warsha na Semina**

| **Kauli** | **Mara moja** | **Zaidi ya mara moja** | **Ambao hawajahudhuria** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya waliohudhuria | 4 (26.7%) | 0 (100%) | 11 (73.3%) | 15 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Matokeo yanaonyesha, kuwa walimu 4 (26.7%) tu ndio wamehudhuria semina au warsha mara moja. Kwa muktadha huo serikali inabidi iongeze rasilimali muda na pesa ili kutoa semina elekezi za kutosha kwa walimu wa shule za sekondari katika wilaya ya Temeke kwani mafunzo na semina mbalimbali ni muhimu kwenye ufundishaji wowote ule. Ili ufundishaji uwe na ufanisi, mwalimu anahitajika kupata mafunzo ya kufundisha ili aweze kulimudu darasa.

### 4.4.4 Umuhimu wa Mafunzo

Katika sehemu hii watafitiwa 4 (26.7%) ambao walihudhuria semina au warsha mara moja, walisema mafunzo hayo yalisaidia kuimarisha uwezo wao katika ufundishaji na kuwaongezea maarifa mapya.

### 4.4.5 Changamoto katika Maandalizi ya Ufundishaji

Katika suala hili, mtafiti alitumia hojaji kuainisha changamoto ambazo walimu hukumbana nazo wakati wa maandali ya ufundishaji. Watafiti wawalipewa nafasi ya

kuamua kwa kuweka tiki kama ni changamoto au siyo changamoto. Mtafiti aliamua hivyo ili kuweza kupata data zaidi katika changamoto zinazowakabili walimu wakati wa maandali ya ufundishaji. Jedwali na. 4.8 linathihirisha:

**Jedwali 4.8 Changamoto Katika Maandalizi ya Ufundishaji**

| **Kauli** | **Ni changamoto** | **Si changamoto** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Urefu wa mada | 10 (66.7%) | 5 (33.3) | 15 (100%) |
| Ukosefu wa nyenzo za ufundishaji | 12 (80%) | 3 (20%) | 15 (100%) |
| Utayari wa wanafunzi | 12 (80%) | 3 (20%) | 15 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Mtafiti alibaini kuwa walimu 10 (66.7%) walisema kuwa urefu wa mada ni changamoto wanayokumbana nayo wakati wa maandalizi ya ufundishaji na 5 (33.3%) hawakukubalina na kauli hii. Walimu 12 (80%) waliafiki kuwa ukosefu wa nyenzo za ufundishaji ni changamoto katika maandalizi ya ufundishaji na 3 (20%) waliona sio changamoto. Watoa taarifa 12 (80%) walisema hukumbana na changamoto utayari wa wanafunzi na walimu 3 (20%) walisema sio changamoto katika maandalizi ya ufundishaji. Mtafiti alitaka watafitiwa kutaja changamoto zingine ambazo hukumbana nazo wakati wa maandali. Walimu 8 (53.3%) walitaja ugumu wa mada ni changamoto ambayo wanakumbana nayo wakati wa maandalini wakati walimu 7 (46.7%) wao walifanana katika majibu na walisema ukosefu wa muda wa kutosha ni changamoto inayowakabili wakati wa maandalizi ya ufundishaji.

Matokeo yanadhihirisha kuwa walimu hawana budi kuongeza jitihada katika maandalizi ili kuboresha ufundishaji kwani walimu wengi wanafundisha Kiswahili

bila ya kuwa na nyenzo za kutosha ndio sababu ya kuwa changamoto inayowakwamisha katika ufundishaji. Mwalimu ni lazima awe mbunifu wa mambo mbalimbali ili weze kuandaa na kutumia nyenzo mbalimbali za ufundishaji kwa mfano, kutumia picha, kutumia vitu halisi, kutumia ishara, ujuzi wa kuchora, kuigiza michezo (igizo) darasani, na kujua teknolojia vizuri ili kuweza kubuni na kuunda viwezeshi mbalimbali ambavyo vitasaidia katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Mwalimu anatakiwa kutumia uwezo wake na ubunifu wa hali ya juu katika maandalizi kwa kuhakikisha anatumia mitindo mbalimbali ili wanafunzi wanashiriki na kufurahia somo.

## 4.5 Maoni ya Walimu, Wanafunzi na Wakuu wa Shule Kuhusu Somo la Kiswahili

Sehemu hii inashughulikia lengo la nne ambalo ni kubaini maoni ya walimu, wanafunzi na wakuu wa shule kuhusu utatuzi wa changamoto za somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Mtafiti alitumia mbinu ya hojaji na usaili ili kuwapa watafitiwa nafasi ya kutoa maoni yao katika kuendeleza na kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Maoni haya yalingawanyika katika sehemu tatu kulingana na watafitiwa.

Maoni ya wanafunzi, maoni ya walimu na mwisho maoni ya wakuu wa shule yaliyolenga lengo la nne la utafiti huu. Maoni ya walimu, wanafunzi na wakuu wa shule yalikuwa muhimu katika utafiti kwani yalisaidia kutupatia data za kutosha kuwasilisha kwa sababu maoni yao yalitoka katika makundi lengwa ya utafiti huu. Sehemu hii imegawanyika katika sehemu ndogondogo kulingana na maswali ya dodoso yaliyofanyika kwa wanafunzi na walimu, pia maswali ya usaili yaliyofanyika

kwa walimu na wakuu wa shule.

### 4.5.1 Maoni ya Wanafunzi Juu ya Somo la Kiswahili

Utafiti huu ulitoa nafasi ya wanafunzi kutoa maoni yao juu ya ujifunzaji wa somo la Kiswahili**.**Wanafunzi walitafitiwa kwa kutumia dodoso. Na ili kuweza kupata maoni yao, sehemu hii iligawanyika katika sehemu tatu, Kama zifuatazo:

#### 4.5.1.1 Kupenda Somo la Kiswahili

Licha ya wanafunzi kutambua changamoto katika ujifunzaji wa somo la Kiswahili, walipata nafasi ya kutoa hisia zao kama wanafurahia ujifunzaji wa somo la Kiswahili au la. Wanafunzi walitoa maoni yao kwa kuamua ndio au hapana. Matokeo yanadhihirisha kuwa watafitiwa 30 (30%) walisema hawalipendi somo la Kiswahili kwa sababu lina mada ngumu na halina nyenzo za ufundishaji na watafitiwa 70 (70%) walitoa maoni yao kuwa wanalipenda somo la Kiswahili. Hunsen (1977) anasema kuwa, wanafunzi wenye maoni chanya kuhusu somo la Kiswahili hupata alama za juu kuliko wale wenye maoni hasi. Vile vile, wanafunzi wenye maoni chanya kuhusu somo hilo, hutumia muda wao mwingi sana kufanya mazoezi katika somo hilo.

Hali hii inaonyesha bado somo la Kiswahili lina changamoto katika kufikia matokeo mazuri. Hata hivyo, kuna wanafunzi wa somo la Kiswahili ambao wanalisoma kwa kuwa ni somo la lazima ila hawalipendi. Serikali na taasisi lazima ziakikishe zinaimarisha morali kwa wanafunzi kupenda somo la Kiswahili kwa kuanzisha mashindano mbalimbali na kuboresha nyenzo za kujifunzia.

#### 4.5.1.2 Changamoto katika Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili

Wanafunzi wameweza kutoa maoni yao juu ya changamoto ambazo hukumbana nazo wakati wa ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Mtafiti alitumia njia ya hojaji kupata taarifa hii. Changamoto hizi ziliainishwa na watafitiwa wakapata nafasi ya kuamua ndiyo au hapana. Matokeo haya yameonyeshwa katika jedwali na.4.9.

**Jedwali 4.9: Changamoto Ambazo Hukumbana Nazo Wakati wa Ujifunzaji**

| Kauli | Ndiyo | Hapana | Jumla |
| --- | --- | --- | --- |
| Uhaba wa nyenzo za ufundishaji | 80 (80%) | 20 (20%) | 100 (100%) |
| Walimu kukosa ustadi wa mada | 0 (0%) | 100 (100%) | 100 (100%) |
| Mada zake ni ndefu | 70 (70%) | 30 (30%) | 100 (100% |
| Walimu kukosa morali wakati wa ufundishaji | 10 (10%) | 90 (90%) | 100 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022).

Kutokana na jedwali na.4.10, matokeo yanaonyesha kuwa, wanafunzi 80 (80%) wanakubali kuwa uhaba wa nyenzo za kujifunzia ni changamoto na wanafunzi 20 (20%) walijibu hapana kwamba sio changamoto. Aidha wanafunzi 100 (100%) waliona suala la walimu kukosa ustadi wa mada sio changamoto katika ujifunzaji. Wanafunzi 70 (70%) walikubali kuwa suala la somo la Kiswahili kuwa na mada ndefu ni changamoto wakati wa ujifunzaji na wanafunzi 30 (30%) wao waliona sio changamoto. Wanafunzi 90 (90%) waliona walimu kukosa morali wakati wa ufundishaji sio changamoto na wanafunzi 10 (10%) wao wanaona ni changamoto ipo wakati wa ujifunzaji. Kwa mujibu wa mhimili wa Nadharia ya Utabia, ni jukumu la mwalimu kuongoza wanafunzi katika kuhakikisha upatikanaji wa nyenzo za kujifunzia ili kuimarisha ufaulu.

#### 4.5.1.3 Changamoto Zingine

Matokeo ya kielelezo na.4.10, yaliweza kutoa nafasi kwa watafitiwa kutoa maoni yao juu ya changamaoto nyingine ambazo wanafunzi hukumbana nazo wakati wa ujifunzaji. Wanafunzi 70 (70%) waliainisha changamoto ya ugumu wa mada na wanafunzi 30 (30%) walibainisha kuwa nukuu au notisi ndefu sana kuwa ni changamoto wakati wa ujifunzaji.

#### 4.5.1.4 Kauli Mbalimbali Kuhusiana na Somo la Kiswahili

Kwa kutumia hojaji, mtafiti alitoa nafasi ya wanafunzi kutoa hisia zao juu ya kauli kadhaa kuhusiana na somo la Kiswahili kwa kutumia kigezo cha nakubali, siwezi kuamua na sikubali. Kielelezo na.4:11 kinadhihirisha maoni hayo.

**Jedwali 4.10 kauli Zifuatazo Kuhusiana Nasomo la Kiswahili**

| **Kauli** | **Nakubali** | **Siwezi Kuamua** | **Sikubali** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| Ni somo gumu | 70 (70%) | 4 (4%) | 26 (26%) | 100 (100%) |
| Mada zake ni ndefu | 70 (70%) | 0 (0%) | 30 (30%) | 100 (100%) |
| Halina nyenzo za kufundishia | 80 (70%) | 5 (5%) | 15 (15%) | 100 (100%) |
| Halina wataalamu | 0 (0%) | 0 (0%) | 100 (100%) | 100 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Wanafunzi 70 (70%) walikubali maoni kuwa somo la Kiswahili ni gumu, Wanafunzi 4 (4%) wao walisema wanashindwa kuamua na wanafunzi 26 (26%) wao walikataa kauli hiyo ya mtafitiwa. Kauli ya somo la Kiswahili kuwa na mada ndefu wanafunzi 70 (70%) walikubali kauli hii na wanafunzi 30 (30%) wao walikataa. Wanafunzi 80 (80%) walikubali somo la Kiswahili halina nyenzo za kufundishia na watafitiwa 20

(20%) walipinga kauli ya hiyo. Watafitiwa 100 (100%) kwa pamoja walikataa kauli ya kuwa somo la Kiswahili halina wataalamu.

Pia kwa kutumia hojaji, watafitiwa walipewa nafasi ya kupendekeza juu ya ufundishaji wa somo la Kiswahili, Wanafunzi 70 (70%) walipendekeza walimu wa somo la Kiswahili wapunguze ugumu wa mada, wanafunzi hawa walienda mbali zaadi kwa kutoa ,mfano wa mada ya sarufi kuwa ni ngumu na wanafunzi 30 (30%) walisema wanaomba nukuu zifupishwe. Utafiti umebaini kuwa changamoto zinazowakabili wanafunzi wakati wa ujifunzaji wa somo la Kiswahili ni nyingi. Hivyo, ili kuimarisha ujifunzaji wa somo la Kiswahili, walimu wakishirikiana na serikali hawana budi kutatua changamoto ili ufaulu wa somo la Kiswahili uweze kuimarika.

### 4.5.2. Maoni ya Walimu

Walimu walitoa maoni yao juu ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Maoni ya walimu yalikuwa muhimu ili kuweza kufikia lengo la nne katika utafiti huu. Mtafiti alitumia hojaji na usaili ili kupata maoni ya walimu.

#### 4.5.2.1 Changamoto zinaoathiri Uelewa wa Wanafunzi wa somo la Kiswahili

Kwa kutumia hojaji, mtafiti alitaka kuchunguza athari za changamoto alizoziainisha. Athari hizo ziligawanywa katika viwango vitatu ambavyo vilimpa nafasi mtafitiwa kuchangua. Viwango hivyo ni kiwango kikubwa, kiwango cha kati na kiwango kidogo. Matokeo yanaoneshwa katika jedwali na. 4.12.

**Jedwali 4:10 Changamoto Zinaoathiri Uelewa wa Wanafunzi wa Somo la Kiswahili**

| Changamoto | Kiwango kikubwa | Kiwango cha kati | Kiwango kidogo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Urefu wa mada | 10 (66.7%) | 4 (26.7%) | 1 (6.7%) | 15 (100%) |
| Ukosefu wa nyenzo za kufundishia | 8 (53.3%) | 4 (26.7%) | 3 (20%) | 15 (100%) |
| Utayari wa wanafunzi | 5 (33.3%) | 6 (40%) | 4 (26.7%) | 15 (100%) |
| Ushindani kutoka lugha za kigeni | 2 (13.3%) | 4 (26.7%) | 9 (60%) | 15 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Data zinaeleza kuwa walimu 10 (66.7%) waliafiki changamoto ya urefu wa mada kwamba huathiri uelewa wa wanafunzi kwa kiwango kikubwa. Walimu 4 (26.7) waliona athari ni kwa kiwango cha kati na mwalimu 1 (6.7%) yeye aliona ni kiwango kidogo. Athari za ukosefu wa nyenzo za kufundishia walimu 8 (53%) walikubali, walimu 4 (26.75) walikubali kwa kiwango ch kati na walimu 3 (20%) walikubali kwa kiwango kidogo. Walimu 9 (60%) waliamini ushindani kutoka lugha ya kigeni ni changamoto kwa kiwango kidogo. Hali hii imethibitishwa pia na Gross (1971) ambaye alisema kuwa walimu wanahitaji kuwa na mtazamo chanya kuhusu maoni ya wanafunzi.

Kwa kutumia mahojiano, mtafiti aliwataka walimu kujibu maoni ya wanafunzi wao juu ya somo la Kiswahili. Watafitiwa walisema kuwa, wanafunzi wanapenda somo la Kiswahili lakini wanatamani baadhi ya mada zirahishishwe na ziwe fupi, kwani zitasaidia wao kuelewa kwa haraka na watakuwa na nukuu chache ambazo hazitawakatisha tamaa katika usomaji.  Kuhusu mtazamo wa wanafunzi wao juu ya somo la Kiswahili walimu 15 ambao ni sawa na 100% walifafanua kuwa wanafunzi

wengi wana mtazamo kuwa somo la Kiswahili ni gumu kwa sababu ya urefu wa baadhi ya mada na hata upungufu wa vitabu vya kiada na ziada. Hivyo huathiri ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa kuwa ufaulu wao unashindwa kuimarika.

#### 4.5.2.2 Mapendekezo ya Suluhisho za Changamoto

Mtafiti alitumia hojaji kutoa mapendekezo juu ya suluhisho za changamoto kadhaa alizozianisha juu ya ufundishaji wa somo la Kiswahili. Watafitiwa walipata nafasi ya kuamua ndiyo au hapana katika mapendekezo hayo. Jedwali na. 4.13: linadhihirisha.

**Jedwali 4.12 Mapendekezo ya Suluhisho za Changamoto**

| **Pendekezo** | **Ndiyo** | **Hapana** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Kuwa na mada fupi | 12 (80%) | 3 (20%) | 15 (100%) |
| Lugha ya Kiswahili kupewa kipaumbele zaidi | 11 (73.3%) | 4 (26.7%) | 15 (100%) |
| Kuboresha nyenzo za kufundishia | 15 (100%) | 0 (0%) | 15 (100%) |
| Kuimarisha utayari wa wanafunzi | 13 (86.7%) | 2 (13.3%) | 15 (100%) |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Walimu 12 (80%) waliona kuwa na mada fupi ni suluhisho na walimu 3 (20%) walijibu hapana. Watafitiwa 15 (100%) walikubali ni vyema kuwe na uboreshaji wa nyenzo za kufundishia kama suluhisho. Walimu 11 (73.3%) waliona lugha ya Kiswahili kupewa kipaumbele ni suluhisho na walimu 4 (26.7%) walijibu hapana. Walimu 13 (86.7%) walichangia kuwa kuimarisha utayari wa wanafunzi ni suluhisho na walimu 2 (13.3%) wao walijibu hapana. Walimu 12 (80%) walipendekeza, kuimarishiwa warsha au semina za mara kwa mara juu ya ufundishaji ili kujenga na kuimarisha umahiri na kuweza kuendana na mabadiliko ya ufundishaji yanayotokea duniani. Walisisitiza serikali na uongozi wa shule

kusimamia semina hizo kwasababu kwa walimu binafsi hawataweza sababu ya gharama. Pia walimu walipewa nafasi ya kupendekeza juu ya njia nyingine ambazo zitaweza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili shuleni. Walimu 3 (20%) walipendekeza somo la Kiswahili liwe na vitabu malumu vya kufundishia kwa sababu vitabu vilivyopo havijajitosheleza hivyo huwalazimu kutumia mtandao kuongezea nukuu zilizo bora zaidi.

### 4.5.3 Maoni ya Wakuu wa Shule

Katika sehemu hii, mtafiti alitumia mbinu ya usaili ili kuwapa watafitiwa nafasi ya kutoa maoni yao juu ya changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari.

#### 4.5.3.1Upatikanaji wa Nyenzo za Kufundishia na Kujifunzia

Kwa kutumia mahojiano mtafitiwa aliomba wakuu wa shule kujibu swali la changamoto katika upatikanaji wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia. Watafitiwa 5 (100%) walisema bado kuna changamoto katika upatikanaji wa nyenzo za kufundishia hasa kwa vitabu vya kiada na ziada. Watafitiwa waliendelea kusema kuwa uongozi wa shule una jukumu la kuhakikisha nyenzo hizo zinapatikana lakini nyenzo hizo ni ghali na hufanya uongozi wa shule kununua kwa idadi ndogo kila mwaka ili kuongeza palipopungua.

Kwa ujumla kuna uhaba wa nyenzo katika shule na hali hii hudidimiza ufaulu wa somo la Kiswahili. Brown (2007) anasisitiza kuwa, dhima kuu ya nyenzo za kufundishia ni kuokoa muda, kuchochea shauku na kumpa mwanafunzi motisha wa

kushiriki katika vipindi. Kwahiyo uhaba wa nyenzo za kufundishia ni suala ambalo lazima litatuliwe ili kuimarisha ujifunzaji kwa wanafunzi wa somo la Kiswahili. Utafiti unadhihirisha kuwa ili ufundishaji wa Kiswahili uweze kuimarika na matokeo yapatikane katika mitihani ya taifa katika wilaya ya Temeke, wakuu wa shule na wizara ya elimu wakishirikiana na wadau wa elimu hawana budi kuhakikisha wanatatua changamoto za upatikanaji wa nyenzo mbalimbali shuleni.

#### 4.5.3.2 Kuwapo kwa Nyenzo za Kujifunzia

Mtafiti kwa kutumia mahojiano, aliwataka watafitiwa kujibu suala la nani huhakikisha kuwapo kwa nyenzo za kufundishia shuleni. Watafitiwa 5 (100%) walifafanua kuwa uongozi wa shule na mwalimu wa somo huwa na jukumu la kuhakikisha kuwapo  nyenzo za kufundishiani, kwa sababu kuna baadhi ya nyenzo ambao ni jukumu la mwalimu kuwa nazo kwa hiyo mwalimu yeyote analazimika kutayarisha nyenzo za kufundishia. Mfano wa nyenzo hizo ni michoro mbalimbali ya kuimarisha ujifunzaji.

Pia watafitiwa walifafanua kuwa, vitabu vya kiada na ziada ni jukumu la uongozi wa shule kuhakikisha vinapatikana ili kuimarisha ujifunzaji ingawa kuna changamoto kadhaa katika kuhakikisha kuwapo kwa nyenzo hizo. Watafitiwa 2 (40%) wao walisema wanakumbana na changamoto ya matoleo ya vitabu katika kuhakikisha kuwapo kwani baadhi ya vitabu havijachapishwa matoleo mapya na huwalazimu kutumia vilivyopo ingawa ni vichache na havikidhi mahitaji. Watafitiwa 3 (60%) walifafanua uhaba wa vitabu vya kiada kwa kuwa hutegemea ufadhiri wa serikali na wahisani ambao ni mpango wa bila malipo.

Kwa mujibu Saunders (1974) anataja kuwa mtu hukumbuka asilimia 10 ya yale anayoyasikia, asilimia 50 ya yale anayoyasikia na kuona na asilimia 90 ya yale anayoyasikia, kuyaona na kuyatenda. Nayo maelezo ya Krashen (1982) yanawiana na mawazo haya kuwa, wajibu wa mwalimu ni mkubwa mno na unavuka mipaka ya darasani. Mwalimu anastahili kuwapa wanafunzi vifaa vya kutosha na vitakavyo wawezesha na kuwapa muongozo wa kujifunza hata wakiwa wenyewe. Hivyo kutokana na upungufu, walimu huchukua jukumu la kutafuta njia mbadala za kupata vitabu vya kufundishia Kiswahili.

#### 4.5.3.3 Ukaguzi wa Nyenzo

Ukaguzi ni njia moja ya kuimarisha ufundishaji wa somo. Mtafiti alitumia maswali ya mahojiano, kuomba wakuu wa shule kujibu suala la ukaguzi wa nyenzo. Matokeo yanaonyesha kuwa watafitiwa 5 (100%) walisema walimu wakuu ndio wenye jukumu la kukagua nyenzo za kujifunzia na kufundishia. Pia mtafiti alitaka kujua ni mara ngapi hukagua nyenzo za ufundishaji. Matokeo yanadhihirisha wakuu wa shule 5 (100%), hukagua nyenzo za kufundishia mara kwa mara sababu matumizi ya nyenzo za kufundishia na kujifunzia huimarisha ujifunzaji.Walieleza kuwa, ukaguzi wa nyenzo ni agizo la Wizara ya Elimu. Walimu wana jukumu la kuhakikisha wanafuata maelekezo ya silabasi ambayo yanamtaka kutumia nyenzo za ufundishaji katika kuimarisha ujifunzaji. Hivyo uongozi ni jukumu lao kukagua nyenzo mara kwa mara ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

#### 4.5.3.4 Maandalizi ya Warsha au Semina

Katika swali la maandalizi ya warsha au semina, watafitiwa 3 (60%) walikuwa wazi kusema ni muda mrefu hawajaandaa warsha au semina za uimarishaji wa ufundishaji

kwasababu ya gharama ingawa ni kitu muhimu kwa walimu. Watafitiwa 2 (40%) walisema huwa wanaandaa warsha za ufundishaji kila mwanzo wa mwaka ili kuimarisha ufundishaji kwa walimu.

#### 4.5.3.5 Maoni ya Wakuu wa Shule Juu ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Kwa kutumia usaili mtafiti aliwataka wakuu wa shule kutoa maoni yao juu ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa watafitiwa 3 (60%) waliomba walimu wa somo la Kiswahili kutumia njia mbalimbali kama uazimaji na mtandao ili kuweza kupata baadhi ya nyenzo za kufundishia kuliko kusubiria hisani ya serikali kwani haitoshelezi mahitaji. Kutokana na changamoto hii, Pollard (2002) anashauri mwalimu kuteua nyenzo ambayo taasisi inaweza kumudu gharama yake.

Utafiti uligundua walimu wakuu 2 (40%) waliwataka walimu kuinua utayari wa wanafunzi ili kuweza kupenda somo la Kiswahili. Pia wakuu wa shule 5 (100%) waliomba serikali kuendelea kudhamini warsha au semina za kukuza na kuendeleza ujuzi kwa walimu wa somo la Kiswahili. Utafiti umebaini kuwa ili kuweza kuimarisha ufundishaji maoni ya wakuu wa shule ni muhimu. Hoja hii inashadidiwa na Urevbu (1999) anayefafanua kuwa wakuu wa shule ni kiungo muhimu hivyo maoni yao huchangia ubora wa utendaji. Hata hivyo, utafiti unashikilia kuwa ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili, walimu wakuu hawana budi kuhakikisha kuwa wanatatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu na wanafunzi wa somo la Kiswahili.

### 4.6 Hitimisho

Sura hii imechambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambao zimepatikana

kwa kutumia mbinu ya hojaji na mahojiano. Uwasilishwaji na uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo ya utafiti mahsusi ya utafiti huu. Nadharia ya Utabia ya Skinner (1957) imesaidia kuchanganua data kwa kuyaweka wazi kwa maswali na majibu ya utafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inajumuisha muhtasari wa utafiti, hitimisho la utafiti na mapendekezo ya utafiti kuhusu changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari. Sehemu ya kwanza ya sura hii inahusu muhtasari, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Katika sehemu hii mtafiti amewasilisha kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Muhtasari wa Jumla

Utafiti huu kwa ujumla ulikusudia kuangazia changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari uchunguzi kifani wilaya ya Temeke. Ili kufanikisha lengo kuu, utafiti ulikuwa na malengo mahsusi manne ambayo nikutathamini changamoto za upatikanaji wa nyenzo za kufundishia kwa walimu wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Lengo la pili lilikuwa kuchunguza changamoto za upatikanaji na matumizi ya nyenzo za kujifunzia kwa wanafunzi wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Lengo la tatu lilikuwa kutathmini ubora wa maandalizi ya walimu kuhusu ufundishaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Lengo la nne lilikuw kubaini maoni ya walimu,wanafunzi na wakuu wa shule kuhusu utatuzi wa changamoto za somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Ili malengo haya yatimie, mtafiti alisawiri maswali na majibu ya watafitiwa kwa kutumia hojaji na mahojiano.

Utafiti huu uliwashirikisha watafitiwa 120 waliotumika kama sampuli wa utafiti huu. Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia madhumuni mahsusi ya utafiti na ulitumia Nadharia ya Utabia ya Skinner, ambapo mtafiti alitumia nadharia hii katika kuangalia jinsi walimu wanavyoweza kufuata mihimili muhimu katika ufundishaji, mfano wa mihimili aliyoisistiza Skinner ni kuimarisha ujifunzaji kwa wanafunzi na kuwa na mazingira mazuri ya ujifunzaji kwa wanafunzi. Mtafiti alitumia mihimili hiyo kuangalia nyenzo za kufundishia na kujifunzia vinavyoweza kuwa changamoto kwa walimu na wanafunzi. Kutokana na matumizi ya nadharia hii katika kusawiri malengo mahususi, mtafiti aligundua bado mazingira ya ujifunzaji kwa wanafunzi ni changamoto kwa sababu nyenzo za kujifunzia ni tatizo ambalo limewasilishwa na watafitiwa.

### 5.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo manne ya utafiti. Malengo hayo yameshughulikiwa ifuatavyo:

#### 5.2.2.1 Changamoto Wanazozipata Walimu katika Ufundishaji wa Somo la Kiswahili

Ufundishaji unaofaa zaidi ni ule unaohusisha zaidi matumizi ya nyenzo za ufundishaji ambavyo humsaidia mwanafunzi kushiriki na kuelewa vizuri somo. Katika hojaji na usaili walimu wengi walionyesha kuwa kulikuwa na uhaba wa nyenzo za kufundishia na hivyo kusababisha changamoto katika ufundishaji. Pia utafiti umebainisha kuwa walimu wanapata changamoto katika utayari wa wanafunzi kwa sababu ya ugumu wa baadhi ya mada hii imetokana na walimu kukosa mafunzo wanapokuwa kazini, mafunzo ambayo yangewafanya walimu kuimarisha ufundishaji

wao katika lugha ya Kiswahili na hata kuwa na ujuzi mbalimbali wa kuandaa kutengeneza viwezeshi ili kutumika katika ufundishaji wa kwenye mada korofi. Jambo hili linatokana na taasisi na Wizara ya Elimu kutoweka mafunzo maalumu ya walimu ya mara kwa mara baada ya kumaliza chuo cha mafunzo ya elimu.

#### 5.2.2.2 Changamoto za Wanafunzi katika Kujifunza Somo la Kiswahili

Aidha, kwa upande wa wanafunzi matokeo yalionesha wazi kuwa sio walimu tu wanaopata changamoto katika kufundisha bali na wanafunzi nao wanapata changamoto katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Matokeo yanaonyesha kuwa, na mada ndefu, ugumu wa mada na kukosekana kwa nyenzo za kufundishia ni changamoto katika ujifunzaji kama ilivyoripotiwa na wanafunzi. Changamoto zingine zilizoripotiwa ni walimu kutunga mitihani migumu ambayo huwasababisha kukata tamaa wanapofeli na huathiri ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

#### 5.2.2.3 Maandalizi ya Walimu kuhusu Ufundishaji wa Somo la Kiswahili

Ili kuendelea kuimarisha utendaji wa mwalimu warsha au semina ni suala muhimu. Utafiti huu umebaini kuwa ni walimu wachache ndio hupata nafasi ya kuhudhuria semina au warsha za kuimarisha uwezo wao. Baadhi ya walimu waliohojiwa walisema kwamba hawakupata nafasi ya kuhudhuria semina au warsha yoyote. Aidha, kwa wale waliohudhuria walibainisha kuwa walihudhuria semina au warsha mara moja tu. Hali ni hatari kwa maendeleo ya somo la Kiswahili kwani huenda ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili usipate mabadiliko katika ufaulu wilaya ya Temeke kwasababu walimu wanashindwa kupata mafunzo mapya au yale ya kuendeleza na kuimarisha uwezo wao katika kuendana na mabadiliko ya ufundishaji.

#### 5.2.2.4 Maoni ya Walimu, Wanafunzi na Wakuu wa Shule Kuhusu Somo la Kiswahili

Walimu wengi wanaomba vitabu maalum ya ufundishaji wa somo la Kiswahili kwani vitabu vilivyopo ni vingi na bado vina mapungufu kwa baadhi ya mada kama vile sarufi. Hivyo wanasema kuwa kutokana na hali hii huwalazimu kuwa na rejea nyingi wakati wa kuandika nukuu ili kutekeleza na kukamilisha silabasi.Wakuu wa shule nao walitoa maoni yao juu ya uhaba wa nyenzo za kufundishia na kuwaasa walimu kuwa na moyo wa kujitafutia nyenzo za kufundishia kwa kuazima au kununua pale shule inapokuwa imekwama katika manunuzi.

## 5.3 Hitimisho

Baada kuchanganua data ya utafiti, mambo mbalimbali yalifichuka. Utafiti ulibainisha kwamba upatikanaji wa nyenzo za kujifunzia bado ni changamoto kwa walimu na wanafunzi. Hali hii husababisha walimu kutotumia nyenzo za kufundishia na hata zinazotumika ni kwa uchache kwa sababu ya idadi iliyopo.  Pia hufanya wanafunzi kutolipenda somo la Kiswahili. Hali hii inadhihirisha wazi kuwa kigezo cha nyenzo za kujifunzia huathiri ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwani ilibainika kuwa shule 3 kati ya 5, hazina maktaba ya kujisomea hivyo kuleta changamoto kwa wanafunzi kujisomea binafsi katika kuongeza maarifa.

Kwa upande mwingine wanafunzi bado wana mtazamo hasi kuhusu somo la Kiswahili kwa sababu wanaona ni somo gumu, lakini ugumu huu unatokana na wanafunzi kukosa nyenzo muhimu za kujifunzia. Vile vile ilibainika kuwa walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari wengi hawahudhuri; kozi za kuwapiga msasa yaani semina au warsha. Hivyo, changamoto hizo zinakwamisha na kuufanya

mchakato wa kujifunza lugha ya Kiswahili kuwa na ugumu. Ili ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili kuwa na ufanisi zaidi na kupunguza changamoto zinazojitokeza, shule za sekondari Temeke na wizara ya Elimu zinashauriwa kufuata mapendekezo yaliyobainishwa katika utafiti huu.

### 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na utafiti huu, mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo:

#### 5.4.1 Mapendekezo ya Kiutekelezaji

Baada ya kutafiti na kuchanganua data, matokeo ya utafiti huu yamebainishwa na mtafiti anatoa mapendekezo kuwa, walimu waimarishe matumizi ya nyenzo za kufundishia ili iwe rahisi kwa wanafunzi kushiriki na kulipenda somo zaidi. Miongoni mwa nyenzo hizo ni vitabu vya kiada na ziada, matumizi ya silabasi na matumizi ya maktaba ambazo humarisha ujisomeaji na maendeleo ya somo la Kiswahili. Katika baaadhi ya nyenzo, walimu ni vyema akahakikisha zinaweza kukidhi idadi ya wanafunzi. Isitoshe inapendekezwa pia kuwepo na kipindi cha matumizi ya maktaba katika ratiba ya ufundishaji ili kuwahimiza wanafunzi kusoma matini yatakayowaongezea umilisi katika somo la Kiswahili na hata kwa shule zisizo na maktaba ni vyema kuwahamasisha wanafunzi kuhudhuria maktaba za serikali kama vile maktaba ya Tanganyika katika kuimarisha uelewa wa baadhi ya mada.

Pia ni vyema walimu wawe na taaluma na ujuzi wa kuweza kuyajua mahitaji ya wanafunzi wao kabla na wakati somo linapoendelea kwa kujenga mtazamo chanya kuhusu somo la Kiswahili kwa wanafunzi kwa ujumla kwa sababu Kiswahili ni lugha ya taifa, lugha rasmi na somo la lazima kwa kidato cha kwanza hadi cha nne.

Baadhi ya wanafunzi wanaonyesha kutopenda somo la Kiswahili na wanaamini ni gumu kwa sababu ya mitihani migumu inayotugwa na walimu, mada zake kuwa ndefu na baadhi ya mada wanaamini ni ngumu. Ni vyema Wizara ya Elimu iweze kufuatilia na kuchunguza namna walimu wanavyofundisha na pia kuakikisha namna ya kurahisisha baadhi ya mada kwa ajili ya kupata matokeo bora ya mitihani ya taifa.

Aidha walimu wakuu wa shule na serikali wanatakiwa kutambua warsha au semina ni kitu muhimu hivyo ni vyema ziandaliwe mara kwa mara kwa kushirikisha wataalamu wa lugha ili kuimarisha ujuzi wa walimu katika ufundishaji wa somo la Kiswahili na kumsaidia kuendana na mabadiliko. Kwa kufanya hivi walimu watapata maarifa ambayo yatatoa ugumu wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi na kuamsha ari ya walimu kutumia nyenzo na kujianda vyema kabla ya kuingia darasani. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa mno katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari.

### 5.4.2 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Mtafiti hawezi kudai kuwa ameshughulikia mambo yote kuhusu changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Itakuwa bora zaidi ikiwa utafiti wa aina hii utafanywa katika maeneo mengine nchini. Utafiti huo unaweza kuwa mlinganisho ambapo matokeo katika maeneo mengine yanaweza kulinganishwa ili kubainisha hali halisi ya changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Utafiti kama huu unaweza kufanyika vilevile katika shule za msingi ili kubaini hali halisi kuhusu changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Mwisho kwa vile utafiti huu ulifanywa kwa wanafunzi wa kidato cha tatu pekee katika wilaya ya Temeke, ipo haja ya utafiti mwingine kufanywa katika vidato

vingine katika maeneo mengine nchini ili kuyalinganisha na matokeo haya na kubaini hali halisi kuhusu changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

**MAREJEO**

Adam, J. na Kamuzora, F. (2008). *Research methods for business and social studies.* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Akaka, L. (2013). "Changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya". *Kioo cha Lugha*, 11 (1) 49-56.

Babusa, H. (2010). *Uchunguzi linganuzi wa mielekeo na umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi katika mikoa ya pwani na Nairobi nchini Kenya.* Nairobi: Kenyatta University.

Balisidya, M. (1987). "Tanzu fani za fasihi simulizi". *Mulika 19*, 11-18.

Bamgbose, A. (2000). *Language and exclusion:The consequence of language policies in Africa.* London: Transaction Publishers.

Barber, C. (1972). *The Story of Language.* London: Pan Books.

Besha, R. (1994). *Utangulizi wa lugha na isimu.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Brock-Utne, B. (2005). *The Continued Battle over Kiswahili as the Language of Instruction in Tanzania.* Dar es Salaam: Mkuki&Nyota Publishers.

Brock-Utne. (2003). *Language of instruction in Tanzania and South Africa*. Dar es Salaam: E&D publishers.

Brown, H. (2007). *Principle of language learning and teaching (5th Ed.) White Plains.* New York: Pearson Education.

Brown, H. D. (2007). *Principle of language learning and teaching.* New York: Pearson Education.

Chomsky, N. (1959). *Review of F.B.Skinner's verbal behavior.In Reading in the psychology of language.* London: Prentice Hall.

Cohen, L. (2007). *Research methods in education.* London: Routledge Falmer.

Creswell, J. (2014). *Research Design:Qualitative,quantitative and mixed methods approches.* California: Sage Publications.

Criper, C and Dodd,W. (1984). *Report on the teaching of english language and its use as medium of education in Tanzania.* Dar es Salaam,Tanzania: The British Council.

Crystal, D. (1997). *The Cambridge encyclepidia of language.* London: Cambridge University press.

Deodutus, R. (2015). *Nadharia za awali katika uamiliaji wa lugha ya pili. Imepakuliwa kutoka www.acd.edu.Toleo la 6/11/2021.*

Fasold, R & Linton, J. C. (2006). "An Introduction to Languages and Linguistics". *Universal Properties of Language* 1-11.

Goffin, S. G., & Wilson C. (2001). *Curriculum models and early childhood education: Appraising the relationship.* (2nd Ed) New Jersey: Merrill/ Prentice Hall.

Hunsen, J. (1977). "International Study of achievent in mathematics. A Comparison of twelve Countries". Chicago Journals *21*, 230-246.

Kothari, C. (2009). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Kothari, R. (2014). *Research Methodology and Methods Techniques(3rd edition).* New Delhi: New Age International (P) LTD.

Krashen, (1982). *Principle and practice in second language acquisition.* New York: Pergamon Press.

Mackey, (2006). Second Language Acquisition. In Fasold, & J. R na Linton, *An*

*Intoduction to Languages and Linguistics*, 433-462. New York: Cambridge University Press.

Malekela, G. (2003). "English as a medium of instruction in post-primary education in Tanzania:Is it a fair policy to the learner?" In B. a. Brock-Utne, *Language of instruction in Tanzania and South-Africa*,102-112.

Masamba, D. (2004). *Kamusi ya Isimu na falsafa ya lugha.*Dar es Salaam: TUKI.

Mbaabu, I. & Nzunga, M. (2008). *Sheng' its major characteristics and impact in standard Kiswahili and English.* Dar es Salaam: TUKI.

Mbunda, F. (1996). *OED 2008: Mbinu za kufundisha lugha ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mekacha, R. (2000). *Isimu jamii-Nadharia na muktadha wa Kiswahili.* Minoocity: Osaka university of foreign studies.

Mligo. (2012). *Jifunze Utafiti:Mwongozo kuhusu utafiti na uandishi wa ripoti yenye mantiki.* Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).

Mochiwa, Z. (1991). "Bifocumlism or Unifoculism in education? A critical evaluation of language policy in Tanzania". In J. Hutchison, *Issues in Language and Education* (pp.1-21.).

Moochi, C. (2013). *Performance differences and gender in Kiswahili creativiy writing. A case study of selected secondary school's in Nyamira.* Nairobi: Nairobi publishers.

Mpemba, T. (2007). *Tanzania policymakers reluctance to sanction, Kiswahili instructional medium in pos-primary education.* Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Msanjila, Y.P (2004). *Kiswahili kitumike kufundishia shule za sekondari na elimu ya*

*juu Tanzania.* Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila, Y.P (1998). "Uzoefu wa kutumia Kiswahili kama Lugha ya kufundishia katika vyuo vya ualimi nchini Tanzania". Journal of *Linguistics and Language in Education* 3(1), 75-95.

Msanjila, Y. P. (2011). *Isimu jamii sekondari na vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Msokile, M. (1992). *Historia na matumizi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Kibaha Printing Press.

Mtembei, I. (1997). *Njia mbili zilimshinda fisi:Tanzania na suala la lugha ya kufundishia.* Dar es salaam: BAKITA.

Mukhawana, M. (1995). Kiswahili sanifu je kipo? *baragumu,* 1(2), 18-25.

Muruguru, S. (2000). *Students' performance in Kiswahili: A Study of selected schools in Nakuru Sub-Country.* Nairobi: Chuo Kikuu cha Moi.

Mwinshekhe, H. (2003). "Using Kiswahili as a medium of instruction in science teaching in Tanzania secondary schools". In Z. Birgit Brock-Utne, *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*,129-148.

Njongu, K. & Nganje, D. K. (2006). *Kiswahili kwa vyuo vya ualimu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Orasanu, J. (2001). *Reading comprehension. From research to practice.* Hillsdale: Lawrence Erlbaum.

O-saki, K. (2003). *Evaluation of lead teacher training institutes in Ethiopia:A consultance report prepared for UNESCO.* Paris: UNESCO.

Pollard, M. (2002). *Effective Teaching*. New York: Teachers College Press

Pretorius, E. (2002). Reading ability & academic performance in South Africa:Are We Fiddling while Rome is burning? *Language Matters*, Issue 33,169-196.

Qorro, M. (2006). *Does language of Instruction Affect Quality of Education.* Dar es salaam,Tanzania: Haki Elimu working papers.

Richards J. C. & Rodgers, T. S. (1986). *Approches and methods in language teaching.* New York: Cambridge University Press.

Riley, J. (2005). *Learning in the early childhood development policy framework.* Nairobi: Government Printer.

Robson, C. (2007). *How to do a research project: A guide for undergraduate Students.* Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Rodgers, S. (1976). *Approaches and Methods in Language Teaching:A Description and Analysis.* Cambridge: Cambridge University Press.

Rubagumya, C. (1990). "Language in Tanzania". In Rubagumya, *Language in education in Africa:a Tanzanian Perspective* (pp. 5-14). Clevedon (UK): Multilingual Matters Inc,.

Rubagumya, C. (1991). Language promotion for education purposes: the example of Tanzania. In K. Legere, *The role of language in literacy programmes with special reference to Kiswahili in eastern Africa* (pp. 198-215). Bonn: Deutsche Stiftung fur Intentionale Entwicklung.

Rubanza, Y. (2002). "Realistic revolutionary strategies in harmonisation and standardisation of African language". In K. K. Prah, *Rehabilitating African Language.* Cape Town: CASAS.

Saleh, F. (2019). *Changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili kama lugha ya kigeni katika darasa msetola wingiugha* . Zanzibar: SUZA.

Saunders, D. (1974). *Visual communication handbook: Teaching and Learning using simple visual material.* London: Lutterworth Press.

Savignon, S. (2005). *Communicative Competence: An experiment in Foreign Language Teaching.* Montreal: Quebec: Marcel Didier.

Senkoro, F. (2004). *Teaching in Kiswahili at university level*: The case of Kiswahili department at the University of Dar es salaam.

Skinner F, B. (1957). *Verbal behavior.* New York: Appleton Century Crofts.

Su,M.J.&Hong,Z.F.(2007).*Professional development of science practice:Application of teaching aids.* London: Paul Chapman Publishing Ltd.

Swilla, I. (2009). Languages of instruction in Tanzania: Contractions between ideology, policy and implementation. *African study monographs,* 30(1): 1-14.

TET. (2016). *Zana za kufundishia kujenga dhana ya namba.* Dar Es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

UNESCO, (1953). *The use of Vernacular language in education.* Paris: United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.

Weber, H. (1985). *Dictionary of applied linguistics.* London: longman.

WEMU, (2014). *Sera ya elimu na Mafunzo.* Retrieved from www.moevt.go.tz

Yorandi, S. (2013). *Lugha ya Kiswahili katika kufundishia na Kujifunzia Elimu na vyuo.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (M.A. Kiswahili).* Dar es Salaam,Tanzania: Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO NA 1: BAJETI

| Na | Maelezo | Gharama |
|---|---|---|
| 1 | Matayarisho ya uandishi wa pendekezo-vifaa vya kuandikia kama vile madaftari, kalamu na rula | 150,000 |
| 2 | Huduma za kompyuta na interneti | 200,000 |
| 3 | Matayarisho za zana za kukusaya data, kutayarisha maswali ya usaili na dodoso | 150,000 |
| 4 | Kukusanya data, usafiri kwa ajili ya kufuata watafitiwa | 250,000 |
| 5 | Uchambuzi wa data | 100,000 |
| 6 | Uandishi wa ripoti | 300,000 |
| 7 | Kuchapa na kutoa ripoti | 400,000 |
| 8 | Usafiri wa kuwasilisha ripoti | 50,000 |
| **Jumla kuu** | | 1,600,000 |

## KIAMBATANISHO NA 2: RATIBA YA KUFANYA UTAFITI

## MPANGO WA KAZI 2021-2022

| Na | Shughuli | MWAKA | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021 | | | | | 2022 | | | | | |
| | | Agus | Sept | Oct | Nov | Dec | Jan | Feb | Mach | Apr | Mei | Juni |
| 1 | Kusoma kazi tangulizi | | | | | | | | | | | |
| 2 | Kuandika pendekezo | | | | | | | | | | | |
| 3 | Kuandaa zana za kukusanyia data | | | | | | | | | | | |
| 4 | Kwenda uwandani na kukusanya data | | | | | | | | | | | |
| 5 | Uchambuzi wa data | | | | | | | | | | | |
| 6 | Uandishi wa ripoti | | | | | | | | | | | |
| 7 | Kuchapisha na kuwasilisha | | | | | | | | | | | |

## KIAMBATANISHO NA 3: HOJAJI YA MWALIMU

Dodoso hili ni kwa ajili ya utafiti unaohusu tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari, wilaya ya Temeke. Unaombwa ujibu maswali haya kwa usahihi kutokana na uelewa wako ili usaidie kutoa matokeo yatakayoleta mabadiliko chanya kwa maendeleo ya Kiswahili.

**Maelekezo:**

- Tafadhali jaza nafasi katika hojaji uliyopewa.
- Hakuna haja ya kuandika jina lako.
- Maelezo utakayotoa yatatumiwa tu kusudi la uchunguzi huu na yatahifadhiwa vizuri wakati wa utafiti na baada ya utafiti

**SEHEMU A: Taarifa binafsi**

Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi

1. Jinsia
    a) Kike (        )
    b) Kiume (          )
2. Kiwango cha elimu
    a) Stashahada/ Diploma (          )
    b) Shahada/ B.ED/B.A   (          )
    c) Uzamili/ M.A  (             )
3. Uzoefu wako kitaaluma ni?
    a) Miaka 0-5  (        )
    b) Miaka 6-10 (       )
    c) Miaka 11-15 (        )

d) Miaka 16 na zaidi (      )

**SEHEMU B: Upatikanaji na matumizi ya nyenzo**

Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi

4. Je, ni nyenzo gani za kufundishia zinapatikana shuleni mwako?

| **Nyenzo** | **Ipo** | **Haipo** | **Ipo lakini haitoshi** | **Ipo lakini haitumiki kwa walimu** |
|---|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | | | | |
| Vitabu vya ziada/ marejeleo | | | | |
| Miongozo ya walimu | | | | |
| Silabasi | | | | |
| Kamusi | | | | |
| Maktaba | | | | |

5. Je, ni sababu au vigezo gani vinavyothibiti au kuathiri uteuzi wa matumizi yako ya nyenzo katika ufundishaji wa somo la Kiswahili? Weka tiki kwenye ndio au hapana

   a) Idadi ya wanafunzi Ndio (      ), Hapana (      )

   b) Urefu wa mada Ndio (      ), Hapana (      )

   c) Ushiriki mdogo wa wanafunzi Ndio (      ) Hapana (      )

   d) Nyinginezo (eleza)……………………………………………………

6. Ni mara ngapi hutumia nyenzo zifuatazo katika kufundisha somo la kiswahili? Weka tiki panapofaa.

| **Nyenzo** | **Mara kwa mara** | **Mara chache** | **Haitumiwi kabisa** |
|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | | | |
| **Vitabu vya ziada** | | | |
| **Miongozo ya walimu** | | | |
| **silabasi** | | | |
| **kamusi** | | | |

**SEHEMU C: Maandalizi ya Mwalimu**

Weka alama ya tiki, kwenye kisanduku sahihi

7. Je, umewahi kuhudhuria semina au warsha juu ya ufundishaji wa somo la Kiswahili

   a) Ndiyo (  )

   b) Hapana (  )

8. Umehudhuria semina au warsha mara ngapi?

   a) Moja (  )

   b) Zaidi ya mara moja (  )

9. Ikiwa jibu lako ni ndiyo, eleza jinsi mafunzo hayo yalivyokusaidia

   …………………………………………………………………………………

   …………………………………………………………………………………

   Ikiwa jibu lako ni hapana, eleza kwa nini hayajakusaidia

   …………………………………………………………………………………

   …………………………………………………………………………………

10. Wewe hujiandaa kabla ya kufundisha somo la Kiswahili?

   (a) Ndiyo

   (b) Hapana

11. (i) Onyesha iwapo zifuatazo ni changamoto ambazo wewe hukumbana nazo katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Weka tiki panapofaa

| **Kauli** | **Ni changamoto** | **Si changamoto** |
|---|---|---|
| Urefu wa mada | | |
| Ushindani kutoka kutoka lugha za kigeni | | |
| Ukosefu wa vyenzo za ufundishaji | | |
| Utayari wa wanafunzi | | |

(ii) Je, zipo changamoto nyingine unazokumbana nazo nje ya hizo hapo juu?ikiwa jibu ni Ndio, zitaje………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

**SEHEMU D: Maoni ya walimu kuhusu somo la Kiswahili**

12. Onyesha ni kwa kiwango gani changamoto zifuatazo zinaoathiri uelewa wa wanafunzi kwa lugha sanifu ya kiswahili. Weka alama ya tiki.

| **Changamoto** | **Kiwango kikubwa** | **Kiwango cha kati** | **Kiwango kidogo** |
|---|---|---|---|
| Urefu za mada | | | |
| Ukosefu za nyenzo za kufundishia | | | |
| Utayari wa wanafunzi | | | |
| Ushindani kutoka lugha za kigeni | | | |

13. Onyesha iwapo mapendekezo yafuatayo ni suluhisho kwa changamoto zinazokabili ufundishaji wa somo la Kiswahili.Weka alama ya tiki.

| **Pendekezo** | **Ndiyo** | **Hapana** |
|---|---|---|
| Kuwa na mada fupi | | |
| Kuboresha njenzo za kufundishia | | |
| Lugha ya Kiswahili kupewa kipaumbele zaidi | | |
| Kuimarisha utayari wa wanafunzi | | |

14. Ni nini maoni yako juu ya ufundishaji wa somo la Kiswahili

……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………….

## KIAMBATANISHO NA 4: HOJAJI YA MWANAFUNZI

Dodoso hili ni kwa ajili ya utafiti unaohusu tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari, wilaya ya Temeke. Unaombwa ujibu maswali haya kwa usahihi kutokana na uelewa wako ili usaidie kutoa matokeo yatakayoleta mabadiliko chanya kwa maendeleo ya Kiswahili.

**Maagizo:**

- Tafadhari jaza katika hojaji uliyopewa.
- Hakuna haja ya kuandika jina lako.
- Maelezo utakayotoa yatatumiwa tu kwa kusudi la uchunguzi huu na yatahifadhiwa kwa umakini wakati wa utafiti na baada ya utafiti

**SEHEMU A:** Taarifa binafsi

1) Jinsia

   a) Msichana ( )

   b) Mvulana ( )

**SEHEMU B:** Matumizi ya nyenzo za kujifunzia

2) Je, ni nyenzo gani za kujifunzia zinapatikana shuleni kwako? Weka alama ya tiki sehemu sahihi.

| **Nyenzo** | **Ipo** | **Haipo** | **Ipo lakini haitoshi** | **Ipo lakini hatumiki** |
|---|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | | | | |
| Vitabu vya ziada/ marejeleo | | | | |
| Kamusi | | | | |
| Maktaba | | | | |
| Michoro | | | | |

3) Ni mara ngapi wewe hutumia nyenzo zifuatazo katika kujifunzia somo la Kiswahili? Weka alama ya tiki panapofaa

| Nyenzo | Mara kwa mara | Mara chache | Haitumiki kabisa |
|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | | | |
| Vitabu vya ziada/ marejeleo | | | |
| Silabasi | | | |
| Kamusi | | | |
| Maktaba | | | |
| Michoro | | | |

**SEHEMU C:** Mielekeo kuhusu somo la Kiswahili

4) (i) Je unafurahia somo la Kiswahili?

a) Ndiyo (  )

b) Hapana (  )

(ii) Ikiwa jibu lako ni Hapana tafadhali elezea ni kwa nini hupendi kiswahili

………………………………………………………………………………

5) Ni yapi maoni yako kuhusu kauli zifuatazo kuhusiana na somo la Kiswahili. Weka tiki panapofaa kukadiri maoni yako kwa kutumia vigezo vifuatavyo: nakubali (KU), siwezi kuamua (SA), sikubali (SI)

| **Kauli** | **KU** | **SA** | **SI** |
|---|---|---|---|
| Halina misamiati ya kutosha | | | |
| Ni somo gumu | | | |
| Mada zake ni ndefu | | | |
| Halina nyenzo za kufundishia | | | |
| Halina wataalamu | | | |

6) (i) Onesha iwapo zifuatazo ni changamoto ambazo wewe hukumbana nazo katika ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Weka alama ya tiki panapofaa

| **Kauli** | **Ndiyo** | **Hapana** |
|---|---|---|
| Uhaba wa nyenzo za ufundishaji | | |
| Walimu kukosa ustadi wa mada | | |
| Mada zake ni ndefu | | |
| Walimu kukosa morali wakati wa ufundishaji | | |

(ii) Je, kuna changamoto zingine unakumbana nazo wakati wa ujifunzaji? Kama Jibu ni Ndiyo, zitaje……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………..

7) Pendekeza maoni yako namna ambavyo ungependa somo la Kiswahili lifundishwe ………………………………………………………..

## KIAMBATANISHO NA 5: MWONGOZO WA USAILI KWA MWALIMU

Katika mahojiano ya moja kwa moja, utaratibu ufuatao wa usaili utamwongoza mtafiti katika kumhoji mwalimu

1. (a) taja nyenzo ambazo wewe hutumia kufundishia somo la Kiswahili

(b) Eleza sababu za kuteua na kutumia nyenzo hizo

(c) Je, nyenzo hizo zinatosheleza ufundishaji wa somo la Kiswahili?

2. (a) Je, umewahi kuhudhuria semina au warsha juu ya ufundishaji wa somo la Kiswahili?

(b) Kama jibu ni ndio, ni mara ngapi umehudhuria?

(c) Nini umuhimu wa semina au warsha uliyohudhuria/ulizohudhuria?

3. (a) Je, wanafunzi wako wana maoni gani kuhusu somo la Kiswahili?

(b)Je, mtazamo wa wanafunzi wako kuhusu somo la Kiswahili, huathiri ufundishaji wako wa somo la Kiswahili?

4. Ni nini kifanyike kuondoa changamoto ulizoziainisha?

## KIAMBATANISHO NA 6: MWONGOZO WA USAILI KWA MKUU WA SHULE

Katika mahojiano ya moja kwa moja, utaratibu ufuatao wa usaili utamwongoza mtafiti katika kumhoji mwalimu mkuu ili kusaidia kupata matokeo chanya katika kukuza na kuendeleza somo la Kiswahili

1. Kuna ukaguzi wowote unafanyika wakati wa ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa mwalimu na wanafunzi ili kubaini matumizi ya nyenzo za ufundishaji na ujifunzaji?
2. Je, ni shule ndio huchukua chukumu la kuakikisha walimu wa somo la Kiswahili wanakuwa na nyenzo za ufundishaji? Au ni jukumu la mwalimu?
3. Je, shule inaandaa warsha au semina za kukuza na kuendeleza ujuzi wa walimu katika somo la Kiswahili? Kama jibu ni Ndiyo, ni mara ngapi kwa mwaka?
4. Je, kuna changamoto zipi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili ambazo kama uongozi umeweza kukumbana nazo?
5. Ni nini kifanyike katika kupambana na hizo changamoto? (toa maoni yako)

# KIAMBANISHO NA. 7: BARUA ZA KURUHUSIWA KUKUSANYA DATA

## THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

***DIRECTORATE OF POSTGRADUATE STUDIES***

P.O.BOX 23409
DAR ES SALAAM, Tanzania
http://23409www.openuniv

Tel: 255-22-2668992/2668445
Ext.2101
Fax:255-22-2668759
E-mail: dpgs@out.ac.tz

**REF: PG201705321** **28rd February 2022**

DIRECTOR
TEMEKE MUNICIPALITY
P.O.BOX
**DAR-ES-SALAAM**

**RE: RESEARCH CLEARANCE**

The Open University of Tanzania was established by an act of Parliament No.17 of 1992, which become operational on the 1st March 1993 by public notice No. 55 in the official Gazette. The Act was however replaced by the Open University of Tanzania Charter of 2005, which became operational on 1st January 2007. In line with the Charter, the Open University mission is to generate and apply knowledge through research.

To facilitate and to simplify research process therefore, the act empowers the Vice Chancellor of the Open University of Tanzania to issue research clearance, on behalf of the Government of Tanzania and Tanzania Commission for Science and Technology, to both its staff and students who are doing research in Tanzania. With this brief background, the purpose of this letter is to introduce to you **NEEMA SAMUEL NDOMBA Reg No: PG201705321** pursing MA-KISWAHILI We here by grant this clearance to conduct a research titled **" Changamoto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la kiswahili katika Shule za sekondari Uchunguzi Kifani wilaya ya Temeke "** He will collect his data in your district between 6rd March 2022 to 8th April 2022

In case you need any further information, kindly do not hesitate to contact the Deputy Vice Chancellor (Academic) of the Open University of Tanzania, P.O.BOX 23409, Dar es Salaam. Tel: 022-2-2668820. We lastly thank you in advance for your assumed cooperation and facilitation of this research academic activity.

Yours Sincerely,

Prof. Magreth Bushesha
**For: VICE CHANCELLOR**
**THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA**